

**AMORIM: UNITED HATUSAJILI JANUARI**
UKURASA 22

**MAFURIKO** ya Kilosa yakwamisha abiria 900 wa treni
UKURASA 3

**VIFAA** vilivyoibwa TANESCO, DAWASA na TRC vyakutwa kiwanda cha ujenzi
UKURASA 8

**MWANAJESHI** aongoza shambulio la kigaidi akiua watu 15 Marekani
UKURASA 19

epaper.ippmedia.com
Nipashe MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

Nipashe
Ijumaa Januari 3, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581911
www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
LIKE & FOLLOW US 0677 020701 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ The nipashe Digital nipashedigital

# Mauaji kigogo CCM

**MWENYEKITI** Wazazi, diwani na wenzao watatu kizimbani... *Ukurasa wa 2*



Washtakiwa katika kesi ya jinai namba 34404 ya mwaka 2024 ya mauaji ya aliyekuwa Katibu wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Kilolo, Christina Kibiki wakitolewa Mahakama ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Iringa baada ya kesi hiyo kuahirishwa hadi Januari 7 mwaka huu. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

## Jussa, wanachama ACT wasema Othman anatosha urais Zanzibar

**Rahma Suleiman na Joyce Lameck**

SIKU moja baada ya Mwenyekiti wa Taifa wa ACT-Wazalendo Taifa, Othman Masoud Othman, kutangaza nia ya kugombea urais wa Zanzibar, baadhi ya viongozi wa chama hicho wamesema "anatosha".

Waliosema Othman ana sifa za kupeperusha bendera ya ACT-Wazalendo kwenye Uchaguzi Mkuu uliopangwa kufanyika Oktoba mwaka huu, wametaja sifa ya uzoefu na uadilifu kama nyenzo itakayokipa chama hicho ushindi.

Othman ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, alitangaza nia ya kugombea urais visiwani humo juzi alipozungumza na wahariri mjini Unguja katika salamu zake za Mwaka Mpya 2025.

**Endelea** Uk. 8

## Warioba amtaja Jaji Werema kaishi na sifa kuu tano za kisheria na uongozi

UKURASA 2

**MICHEZO** **YANGA: AMA ZAO, AMA ZETU** UK. 24 **KATUNI** UK. 6

## Mauaji kigogo CCM:

# Mwenyekiti Wazazi, wenzao watatu kizimbani

**Na Francis Godwin,** IRINGA

WATU watano wamefikishwa mahakamani wilayani Iringa kwa mashtaka ya mauaji ya aliyekuwa Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kilolo, Christina Kibiki.

Miongoni mwa washtakiwa hao, wamo Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM Wilaya ya Kilolo, Hedikosi Kimwaga na Diwani wa Nyanzwa, wilayani Kilolo, Boniphace Katili.

Washtakiwa hao walipandishwa kizimbani jana saa nane mchana mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Iringa, Rehema Mayagilo huku ulinzi ukiwa umeimarishwa katika viwanja vya mahakama hiyo.

Akisoma hati ya mashtaka katika kesi hiyo ya jinai namba 34404 ya mwaka 2024 ya mashtaka ya mauaji, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Sauli Makori alidai mahakamani huko kuwa washtakiwa hao; Kefa Wales, Silla Kimwaga, Boniphace Katili, Willy Chikweo na Hedikosi Kimwaga, kwa pamoja wanashtakiwa kumuua Christina Kibiki.

Alidai kuwa watuhumiwa hao walitenda kosa hilo la mauaji Novemba 12, 2024 katika kijiji cha Ugwachanya, wilayani Iringa.

Hata hivyo, Makori alidai upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika. Mahakama iliahirisha kesi hiyo hadi Januari 7 mwaka huu, kesi hiyo itakapotajwa tena.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*




Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi (wanne kulia) akiondoa pazia kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa barabara ya Kizimbani hadi Kiboje na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar Dk Khalid Salum Mohammed (kushoto) ikiwa ni shamrashamra za Maadhimisho ya Miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Warioba amtaja Jaji Werema kaishi na sifa kuu tano za kisheria, uongozi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewaongoza viongozi na wananchi katika mazishi ya Jaji Fredrick Werema, Waziri Mkuu mstaafu, Jaji Joseph Warioba akimwagia sifa kuu tano za kisheria na uongozi.

"Alikuwa mtu mwenye msimamo, akiamini kitu anafanya na kutenda vilevile. Hakuwa na lugha za kuchanganya, alikuwa mwadilifu na alitumikia taifa kwa uwezo wake wote," Jaji Warioba amesema.

Ilikuwa katika tukio la kuaga mwili wa Jaji Werema kwenye viwanja vya Karimjee, jijini Dar es Salaam jana.

Warioba alisema kuwa Jaji Werema atakumbukwa kwa mengi katika utumishi wake wa umma.

Wasifu huo uliendana na kilichoelezwa na aliyemteua katika nafasi ya kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kipindi cha kuanzia mwaka 2009 hadi 2014, Rais Mstaafu Jakaya Kikwete.

Mkuu huyo wa nchi mstaafu alimwelezea Jaji Werema kuwa mwanasheria mbobevu; mzalendo wa dhati na mara zote alitoa ushauri makini uliozingatia maslahi ya taifa huku akimtaja kuwa mahiri na mpenda haki.

"Amefanya mengi mema kwa taifa na ameacha alama ya kudumu nchini. Nilimteua kuwa jaji kutokana na sifa zake katika utendaji," Kikwete alisema.

Waziri Mkuu Majaliwa katika tukio hilo, aliyemwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan, alieleza masikitiko ya Mkuu wa Nchi wa sasa aliyeworodheshea wasifu wa Jaji Werema kuwa kiongozi shupavu, aliyekuwa mwadilifu na mwenye msimamo wakati wote wa utendaji kazi wake.

"Mheshimiwa Rais anajua kwamba Jaji Werema alifanya kazi katika mihimili yote na ana uzoefu mkubwa wa utendaji katika mihimili yote, mengi mazuri ameyatenda.

"Rais Samia anawasihi wote muwe wavumilivu katika kipindi hiki kigumu na ametusihi tuendelee kumwombea na kuenzi yote aliyoyafanya katika utumishi wake," alisema.

Waziri Mkuu alitumia fursa huyo kuwataka wanasheria na watanzania kwa ujumla kuenzi na kuendeleza yale yote mazuri aliyofanya Jaji Werema enzi za uhai wake.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari alisema kuwa Jaji Werema alikuwa mtu mwenye maono na mtaalam wa sheria aliyejitolea na kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha sheria na haki zinatumika katika kuleta maendeleo kwa taifa.

"Jaji Werema alifanya maboresho makubwa katika mfumo wa sheria na haki na alifanikiwa kwa kiasi kikubwa kuboresha na kuimarisha utawala wa sheria na kuwaendeleza, kuwafunda na kuwanyanyua wanasheria waliokuwa wanachipukia, alionesha uongozi wa aina yake katika nyakati ngumu pia aliweza kupigania maslahi ya taifa," alisema.

Wakili Mkuu wa Serikali, Dk. Ally Possi alisema kuwa Jaji Werema alikuwa mahiri na nguzo imara katika sekta ya sheria nchini kwa kuwa aliendelea kutoa huduma katika sekta ya sheria hata baada ya kumaliza muda wake wa utumishi serikalini.

"Uimara wake katika maeneo mbalimbali ya sheria na uchapakazi wake vimeacha alama katika sekta ya sheria nchini," Dk. Possi alisema.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# Trafiki Mbeya wakusanya bilioni 3.4/- mwaka mmoja

**Na Grace Mwakalinga**

JESHI la Polisi limekusanya zaidi ya Sh. bilioni 3.4 kutokana na makosa mbalimbali ya ukiukwaji sheria za usalama barabarani mkoani Mbeya katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba 2024.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, SACP Benjamin Kuzaga alisema makusanyo hayo ni sawa na ongezeko la Sh. milioni 104.8 kulinganisha na makusanyo ya mwaka 2023 ambao walikusanya Sh. bilioni 3.3.

Kamanda Kuzaga alisema makusanyo hayo yamepatikana kutokana na makosa 115,216 ya ukiukwaji sheria za usalama barabarani yaliyoripotiwa mwaka 2024, yakiwa yamepungua kwa makosa 604 kulinganisha na mwaka 2023 ambao ulikuwa na makosa 115,820 yaliyorekodiwa.

Katika taarifa hiyo, Kamanda Kuzaga alisema madereva 28 walifungiwa leseni kwa makosa hatarishi ya usalama barabarani, ikiwa ni pamoja na mwendo kasi, kuyapita magari mengine kwenye maeneo hatari na kusababisha ajali za vifo na majeruhi. Madereva 29 walifikishwa mahakamani kwa ukiukwaji sheria hizo.

Kamanda Kuzaga alitaja mafanikio mengine ya kiusalama mwaka 2024, akisema kuwa watuhumiwa 9,985 walikamatwa kwa makosa mbalimbali ya jinai na kufikishwa mahakamani.

Alisema kuwa jumla ya makosa ya jinai yaliyoripotiwa mwaka 2024 ni 22,049, yakiwa yamepungua kwa makosa 1,705 kulinganishwa na mwaka 2023 ambao ulikuwa na makosa 23,754 yaliyoripotiwa.

Kamanda Kuzaga pia alisema walikamata madini aina ya dhahabu yenye uzito wa kilogramu tisa na gram 622.76, yenye thamani ya Sh. bilioni 1.5.

Alisema madini hayo yalipatikana baada ya watuhumiwa sita kukamatwa. Nyara za serikali zenye thamani ya Sh. bilioni 288.9 zilikamatwa na watuhumiwa 31 walikamatwa (wanaume 29 na wanawake wawili).

Kamanda Kuzaga pia alieleza kuwa wahamiaji haramu 60 walikamatwa kutoka katika nchi za Ethiopia (43), Malawi (15), Burundi (1) na Rwanda (1). Silaha 12 na risasi 63 pamoja na baruti kwenye makopo madogo matatu zilikamatwa katika msako wa kiusalama.

Kamanda Kuzaga alitoa wito kwa wananchi kuendelea kushirikiana na vyombo vya usalama katika kubaini na kuzuia uhalifu kwa kutoa taarifa kuhusu wahalifu, ili hatua stahiki zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kukamatwa kwa wahusika.

## HABARI KITAIFA

# Zaidi abiria 900 wakwama mawasiliano reli kukatika

**Na Paul Mabeja,**
DODOMA

ABIRIA 901 na watumishi 30 wanaosafiri na treni kutoka mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora kwenda Dar es Salaam, juzi walikwama kwa zaidi ya saa sita kwenye kituo kikuu cha reli Dodoma baada ya mawasiliano ya Reli ya Kati kukatika.

Eneo lililokatika mawasiliano ni Godegoge wilayani Mpwapwa na Kidete, wilayani Kilosa, baada ya kujaa maji kutokana na mvua inayoendelea kunyesha maeneo mbalimbali nchini.

Adha hiyo imewakumba abiria waliokuwa wanatoka Dar es Salaam kwenda mikoa ya Kanda ya Ziwa Magharibi na kuulazimu uongozi wa Shirika la Reli nchini TRC, kukodi mabasi ili kusaidia wasafiri hao kuendelea na safari.

Mbwana Omary, mmoja wa abiria hao akizungumza na waandishi wa habari katika Stesheni Kuu ya Dodoma, alisema wametoka mkoani Kigoma juzi na kuwasili Dodoma jana usiku majira ya saa 7:00 usiku.

"Tumeanza safari kutoka Kigoma Desemba 31, lakini njiani tumekuwa na vituo vingi sana kila eneo tunasimama sana, lakini hapa Dodoma tulifika majira ya saa 7:00 usiku na kukaa kwa muda mrefu tulipouliza tukaambiwa tusubiri tutaambiwa nini kinaendelea.

"Tunashangaa asubuhi tunaambiwa kuwa tunaletewa mabasi kwa ajili ya kutuchukua kutuvusha eneo lenye changamoto hiyo na sisi wengine tulitaraji kuwahi mabasi yetu ya mapema, lakini hadi sasa tumeshakosa usafiri, kama mimi na wenzangu tunakwenda Tanga muda huu hatuwezi kupata usafiri tena," alisema.

Aidha, alisema kukwama kwa treni kumeawathiri kwa kiasi kikubwa kutokana na kuongezeka kwa baadhi ya gharama na kuiomba serikali kulifanyia kazi eneo hilo ambalo limekuwa kero kila mwaka.

"Hapa tulipo tayari tumetumia gharama kubwa na tangu tumekwama hapa usiku ule wa saa 7:00 hakuna huduma za msingi ambazo tumezipata," alisema.

Zuwena Juma alisema wanawake pamoja na watoto wamepata usumbufu mkubwa kutokana na kukwama kawa treni hiyo kutokana na kukosa huduma za masingi.

Aliishauri serikali kutafuta mwarobaini ambao utasaidia kukabili hali hiyo ambayo imekuwa kero kwa abiria kila mwaka.

"Hili tatizo sio kama serikali hailifahamu kwani kila mwaka la mvua zitakapoanza kunyesha linatokea, hivyo serikali itafute namna ya kulikomesha hata kama kujenga daraja ili kuwaondolewa usumbufu Watanzania wanaotumia usafiri huu," alisema.

Mkuu wa Stesheni ya Dodoma, Festo Mgomapayo alisema walisitisha safari ya treni hiyo baada ya kupata taarifa kutoka kwa maofisa wao kuwa njia imejaa maji katika eneo hilo kutokana na mvua.

"Treni hii ilingia mkoani Dodoma kutoka Kigoma jana (juzi) usiku wa saa 8:00 na ilipofika hapa tayari tulishapata taarifa za njia yetu kujaa maji kutokana na mafuriko hivyo tusingweza ruhusu iendelee na safari wakati maji yamejaa kwenye njia hadi maji yapungue ili njia ionekane.

"Lakini leo (jana) asubuhi makao makuu wakaamua kuwa hawa abiria wasiendelee kubaki tu hapa hivyo yakakodiwa mabasi ambayo yatawabeba kwa ajili ya kuendelea na safari katika mikoa wanakokwenda.

"Pia, kuna treni yetu nyingine ambayo imezuiliwa kule Kilosa kwahiyo hawa wataenda kuitumia ile ya Kilosa kwenda Dar es Saalam na wale wengine wataletwa na mabasi haya hapa Dodoma kuendelea na safari katika mikoa hiyo ya Kanda ya Ziwa," alisema Mgomapayo.

Wakati huo huo, kesi ya uhujumu uchumi inayowakabili washtakiwa watatu kwa kosa la kuingilia miundombinu ya SGR kwa kutoa vitu muhimu, kuharibu na kuiba nyaya za shaba zenye urefu wa mita 10 zikiwa na thamani ya Dola za Kimarekani 38,581 (Sh. milioni 89.8) imeahirishwa hadi Januari 14, 2025.

Kesi hiyo iliahirishwa jana na Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Dodoma, Eligy Magalla, kutokana na hakimu ambaye alikuwa akisikiliza shauri hilo, Hakimu Mkazi Mfawidhi Denis Mpelembwa kuwa na udhuru.

Washtakiwa hao ni Said Kapambwe mnyamwezi (38) mfanyabiashara mkazi wa Bahi, mshtakiwa wa pili ni Michael Ngayo Legayseki maarufu 'Yakobo Mmasai' (27) mlinzi mkazi wa Bahi Sokoni na mshtakiwa wa tatu ni Petro Merungwa Rengaisi (22), mlinzi mkazi wa Bahi.

Akiwasomea hati ya mashtaka yanayowakabili washtakiwa hao Wakili wa Serikali Zubeda Lyaumi, alisema inadaiwa kuwa Oktoba 7, 2024 maeneo ya Bahi Sokoni, Wilaya ya Bahi, mkoani Dodoma watuhumiwa hao waliingilia miundombinu ya reli ya kisasa (SGR) kwa kutoa vitu muhimu, kuharibu na kuiba nyaya za shaba zenye urefu wa mita 10.

Awali, Wakili wa Serikali Josephat Mwinra, alidai upelelezi bado haujakamilika na kuiomba mahakama kuipangia tarehe nyingine.

Mshtakiwa namba moja Kapambwa anatetewa na Wakaili Meshack Ngamando aliiomba mahakama hiyo kuharakisha uchunguzi kwakuwa shauri hilo halina dhamana.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akitoa heshima za mwisho mbele ya jeneza lililobeba mwili wa aliyekuwa Mwanasheria Mkuu (mstaafu) Jaji Frederick Werema, alipomuwakilisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika maombolezo na kuaga mwili wa marehemu Jaji Werema kwenye viwanja vya Karimjee jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
03.01.2025

## TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa kuanzia siku ya Jumapili **tarehe 05-01-2025** hadi **tarehe 10-01-2025** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea Tunduma kupitia Mikumi, gari hizo zina namba za usajili:

| | | |
|---|---|---|
| **T 204 DYJ /T 630 AJA** | **T 278 EDD /T 269 DUH** | **T 112 EAG /T 837 DJB** |
| **T 458 DYG /T 272 DUH** | **T 678 DUB /T 273 DUH** | **T 116 EDS /T 887 DJB** |

Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 25.00**
**Upana - mita 4.20**
**Kimo - mita 5.20**

2. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam,** hadi **Tunduma** kupitia **Mikumi,** gari zitasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**





MAKALA

NURU AWADH:

# Mwenyekiti mpya wa mtaa aliyeshinda vikwazo vya mfumo dume katika siasa

## -Kuweka ofisi yake chini ya mkorosho kimkakati

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

SIKU ya pili baada ya kura za maoni za Chama Cha Mapinduzi (CCM), niliumwa sana! Kila aliyekuja kuniona, aliniambia niachie hii nafasi mwanamume aingie kufanya kampeni maana huu ugonjwa ninaoumwa si hali ya kawaida," anaeleza Nuru Awadh, Mwenyekiti mpya wa mtaa wa Miembesaba B, kata ya Kongowe wilayani Kibaha.

Nuru (33) anasimulia kuwa haikuwa kazi rahisi kwake kumshawishi kila mtu ili amwelewe, lakini akashikilia msimamo wake wa kuendelea na matibabu huku akisubiri ufike muda wa kampeni nafasi yake Mwenyekiti Mtaa wa Miembesaba B.

"Niligombea kura za maoni tukiwa wanawake wawili na wanaume watano. Nilikatishwa tamaa na wengi, wakidai mimi mwanamke siwezi kuongoza wanaume, lakini nikapuuza maneno yao, wengine walisema nina asili ya kiarabu, sikukata tamaa," anasimulia.

Nuru ambaye aliongoza kwenye kura za maoni CCM kwa kupata kura 139, akifuatiwa na mtiania mwanaume aliyepata kura 113, alipogombea na vyama vingine kuwania nafasi hiyo, akatangazwa mshindi kuwa mwenyekiti wa mtaa huo.

"Baada ya ushindi ndani ya chama changu, uchaguzi ambao ulifanyika Oktoba 23, nilifuatwa nikitakiwa kuachia nafasi kwa mitazamo ya kuwa mtaa huo haustahili kuongozwa na mwanamke.

"Wakati ninaumwa kwa wiki nzima, nilikuwa sina uwezo wa kutoka ndani, hakuna mtiania mwenzangu ndani ya chama aliyefika kunijulia hali na hata wananchi waliofika, wimbo ulikuwa mmoja wakihusisha ugonjwa wangu na mambo ya ushirikina baada ya kuongoza kwenye kura," anasimulia.



Nuru Awadh

**WAKATI WA KAMPENI**

Nuru anaeleza kuwa wakati wa kampeni alipata nafuu ya maradhi yaliyokuwa yanamsibu, akifanya kampeni kwa kushirikiana na wanachama na viongozi wake wa mtaa na kata ya Kongowe kuomba kura.

Katika kampeni zake, mama huyo wa watoto watatu ambaye awamu iliyopita alikuwa mjumbe wa serikali ya mtaa huo, alinadi sera zake, akiahidi kutatua kero alizozitaja kuwa kikwazo kwa wananchi kufanya shughuli zao.

Anasema uhitaji wa zahanati, barabara na ofisi ya mtaa ni vitu ambavyo alisisitiza zaidi kwa wananchi, akiwaomba wamchague ili ashirikiane na viongozi wengine kupata majawabu.

"Mtaa wetu hauna zahanati, nitashirikiana na wananchi tujenge ili wasitumie gharama kwenda kufuata huduma za afya mbali na wanapoishi.

"Nitashirikiana pia na viongozi wangu, akiwamo diwani wa Kongowe kufuatilia kwa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mjini (TARURA) barabara yetu ifanyiwe ukarabati iweze kupitika wakati wote.

"Kitu kingine kilichonipa ushindi ni kunadi kwa wananchi kusudi langu la kujenga ofisi ya mtaa ambayo itarahisisha utoaji huduma kwa wananchi ambao kwa sasa wanatumia ofisi ya ofisa tarafa.

"Mtaa wetu hauna ofisi na mimi nitafanya kazi chini ya mkorosho kutoa huduma kwa wananchi. Tutaweka meza na viti nje. Kwa kufanya hivi, msukumo utakuwapo kwa wananchi kuchangia ujenzi wa ofisi yao na tutakapoishia tutaomba msaada kwa serikali itusaidie kumalizia," anasema.

**BAADA YA UCHAGUZI**

Kampeni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024 zilifikia tamati Novemba 26 na uchaguzi wenyewe ukafanyika Novemba 27, Nuru akiwa tayari ameshazunguka katika kaya 1,655 na kufanya mikutano, akiomba wananchi wake wamchague kuongoza mtaa huo.

Nuru aliibuka mshindi na kutangazwa kuwa mwenyekiti baada ya kupata kura 927 akimshinda mpinzani wake kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ambaye alipata kura 191.

Anasema haikuwa kazi rahisi kupata nafasi hiyo kwa kuwa walio wengi walikuwa wakimkatisha tamaa kuwa hawezi kupata nafasi hiyo kwa kuwa ni mwanamke na mwenye asili ya kiarabu, hivyo hawezi kukubalika kwa wenyeji wa mtaa huo.

Akizungumzia ushindi wake, Nuru anasema vipaumbele vyake alivyonadi kwa wananchi ndivyo vilivyompata nafasi hiyo, pia ujasiri na kutokata tamaa.

"Vikwazo kisiasa kwa wanawake ni vingi ambavyo vikimkuta mtu ambaye hana uvumilivu, anaweza kujitoa kwenye nafasi anayogombea.

"Wanawake wanatakiwa kuondokana na dhana ya woga wa kugombea nafasi za uongozi kwa kuhofia ukabila, udini na imani za ushirikina. Kwa kufanya hivi tutakuwa na viongozi wengi katika ngazi tofauti," anasema Nuru.

Mwenyekiti huyo wa Mtaa wa Miembesaba B pia anawashauri wanawake ambao ni viongozi, wawe mashuhuda kwa wengine ili kuwapa ujasiri wa kugombea na kuwaondolea woga uliojengeka miongoni mwao, hata unawafanya washindwe kuingia katika uongozi.

Katika harakati zote hizo, Nuru anasema mumewe pia amekuwa anampa ushirikiano kuanzia alipochukua fomu hadi sasa.

**WADAU WALONGA**

Mwandishi wa makala hii alifuatilia kampeni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024. Akifungua kampeni hizo, Mbunge wa Kibaha Mjini, Sylvestry Koka alimzungumzia Nuru, akimpongeza kwa uchapakazi wake akiwa mjumbe wa serikali ya mtaa.

"Nuru ni mpambanaji, sina shaka naye na kila alichoahidi kwenye eneo lake tutashirikiana viongozi kutekeleza, hakuna kitu kinashindikana kwa serikali hii inayoongozwa na mama na hapa tunakwenda kumchagua mama," alisema.

Diwani wa Kongowe, Hamis Shomari, akiwazungumzia wanawake waliogombea na kupata nafasi katika kata hiyo, anasema kutokana na uzoefu walionao wenyeviti hao, hana shaka na utekelezaji ahadi walizotoa.

Shomari anasema kuwa kati ya mitaa sita ya kata hiyo, mitatu hivi sasa inaongozwa na wenyeviti wanawake ambao ni pamoja na Nuru Awadh (Miembesaba B), Mboni Mkomwa (Bamba) pamoja na Maimuna Sultani (Kongowe).

Anabainisha kuwa kabla ya uchaguzi huo, Nuru na Mboni walikuwa wajumbe wa serikali za mitaa yao huku Maimuna ambaye amechaguliwa kuwa mwenyekiti wa mtaa huo kwa kipindi cha tatu.

TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

# MWITO WA KUTOA MAONI KUHUSU MAOMBI YA VIBALI VYA UJENZI NA LESENI KUTOKA EWURA

***Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili.***

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 126 (1) cha sheria hiyo kinamtaka mtu yoyote anayetaka kujenga miundombinu ya mafuta kuomba kibali cha ujenzi kutoka EWURA. Aidha, Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

EWURA imepokea maombi ya vibali vya ujenzi na leseni kutoka kwa waombaji walioorodheshwa hapa chini. Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba vibali vya ujenzi ili wajenge miundombinu ya mafuta na leseni kwa ajili ya kujihusisha na biashara/shughuli katika mkondo wa kati na chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Ombi la Leseni/Kibali cha Ujenzi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Salmo Oil Limited, S. L. P 732, Kigoma. | Kiwanja Na. 5, Eneo la Visiga, Kibaha, Pwani. | Mohamed Nassor Ally (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 2. | Salmo Oil Limited, S. L. P 732, Kigoma. | Kiwanja Na. 65, Kitalu "Z", Eneo la Maili 35, Kibaha, Pwani | Mohamed Nassor Ally (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 3. | Backtown Transport Company Limited, S. L. P 16476, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 6, Kitalu "J", Pingo, Chalinze, Pwani. | Hussein Riadha Talecky (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 4. | Yusufu Shabani Omari, S. L. P 45192, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. P16813, Eneo la Temeke Dovya, Temeke, Dar es Salaam. | Yusufu Shabani Omari (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 5. | Firmat Leonard Tarimo, S. L. P 53062, Dar es salaam. | Kiwanja Na. 362, Kitalu "BP", Eneo la Ihumwa, Dodoma. | Firmat Leonard Tarimo (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 6. | Calvin Haleluya Kessy, S. L. P 3073, Dodoma. | Kiwanja Na. 2533, Kitalu "D", Eneo la Iyumbu, Dodoma. | Calvin Haleluya Kessy (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 7. | Lumuma Filling Station, S. L. P 465, Dodoma | Eneo la Lumuma, Kilosa, Morogoro. | Lucas Titus Kipala (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 8. | Chotara Filling Station, S. L. P 1028, Uyui. | Eneo la Katunda, Uyui,Tabora. | Maganga Jaffari Saidi (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 9. | Omegera Company Limited, S. L. P 345, shinyanga. | Kiwanja Na. 1066, Kitalu "S", Eneo la Mwendakulima, Kahama, Shinyanga. | George Marwa Migera (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 10. | XTRA Energies Company Limited, S. L. P 13656, Dar es Salaam. | Eneo la Sokota, Temeke, Dar es Salaam. | Bilal Nahdi (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya Mafuta |
| 11. | SKEU Investment Company Limited, S. L. P 6678, Dar es Salaam. | Jengo la PPF, Ghorofa ya 12, Mtaa wa Samora, Dar es Salaam. | Stellah Kabaka Melkiony (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya Mafuta |
| 12. | S Energies Limited, S. L. P 222, Dar es Salaam. | Eneo la Ilala, Dar es Salaam. | Sharath Krishna Gottipat (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya Mafuta |
| 13. | Olympic Petroleum (T) Ltd, S. L. P 16484, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1002, Kitalu "1", NHC-Kashai, Kinondoni, Dar es Salaam. | Ally Adon (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya Mafuta |
| 14. | Nyati Mineral Sands Limited, S. L. P 105009, Dar es Salaam. | Eneo la Mwasonga, Kigamboni, Dar es Salaam. | Heri Issa Gombera (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta kwa Matumizi Binafsi |
| 15. | ATN Petroleum Co. Ltd - Pugu Filling Station, S. L. P 683, Morogoro. | Kiwanja Na. 2107, Kiwanja "A", Eneo la Pugu Mwakanga, Ilala, Dar es Salaam. | Abdulatif Taalib (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 16. | Sunday Severine Muhobuta T/A SUNCOM Oil Limited, S. L. P 76665, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 74, Kitalu "X", Kisauke, Saranga, Ubungo, Dar es Salaam | Sunday Severine Muhobuta (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 17. | Lake Oil Ltd - Lakeoil Mtoni Kijichi, S. L. P 5055, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 23, Kitalu "G", Mtoni Kijichi, Temeke, Dar es Salaam. | Ally Edha Awadhi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 18. | Victoria Service Station Limited, S. L. P 75467, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 35, Ursino North, Victoria, Temeke, Dar es Salaam. | Harold Elisamehe Matembe (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 19. | Doreen Enterprises Ltd, S. L. P 32874, Dar es Salaam. | Eneo la Ubungo Kibangu, Ubungo, Dar es Salaam. | Steeve Omary Shayo (Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji wa Gesi ya Kupikia (LPG) |
| 20. | GF Vehicle Assemblers Limited, S. L. P 22692, Dar es Salaam. | Eneo la TAMCO-Kibaha, Pwani. | Imran Mehboob Karmali (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya Vilainishi (*Lubricants*) |
| 21. | Afrisian Ginning Ltd, S. L. P 19964, Dar es Salaam. | Eneo la Misugusugu, Kibaha, Pwani. | Samir Abdulwahid (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta kwa Matumizi Binafsi |
| 22. | Njara Company Limited, S. L. P 18059, Dar es Salaam. | Kijiji cha Mzenga, Kisarawe, Pwani. | Tukusuma Paul Samagimila (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 23. | Calvary Filling Station, S. L. P 30153, Kibaha. | Kijiji cha Bokomnemera, Kibaha, Pwani. | Bildard Rogathe Lema (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 24. | Acer Petroleum (T) Ltd-Kilwa Njia Nne, S. L. P 78845,Lindi. | Kiwanja Na. 11, Kitalu "A", Eneo la Njia Nne, Kilwa, Lindi. | Attul Mital (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 25. | Tanganyika Wattle Company Limited, S. L. P 'Private Bag' Njombe. | Shamba Na. 826, Njombe. | Jaswant Singh Rai (Raia wa Kenya) | Leseni ya Kituo cha Mafuta kwa Matumizi Binafsi |
| 26. | Nuru Elisha Mengo – NM Filling Station, S. L. P 166, Matamba - Chimala. | Kijiji cha Matamba, Makete, Njombe. | Nuru Elisha Mengo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 27. | Asamoil Company Limited, S. L. P 15730, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 20, Eneo la Viwanda, Mbinga, Ruvuma. | Azhad Soud Albusaidy (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 28. | Felisiani Selestin Mgaya T/A Mgaya Tiles, S. L. P 761,Songea. | Kiwanja Na.282, Kitalu "FF", Msamala, Songea,Ruvuma. | Felisiani Selestin Mgaya (Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji Gesi ya Kupikia (LPG) |
| 29. | Kilimanjaro Truck Company Limited, S. L. P 80478, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 228, Mpemba, Tunduma, Momba, Mbeya | Rowland Patrick Sawaya (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 30. | FR Star Filling Station, S. L. P 33, Kahama. | Kiwanja Na. 1862, Kitalu "P", Eneo la Mbulu, Kahama, Shinyanga. | Fabian Yohana Ndababonye (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 31. | Olympic Petroleum (T) Ltd - Kigoma, S. L. P 6185, Mwanza. | Kiwanja Na. 14, Kitalu "A", Eneo la Ujenzi, Kigoma CBD, Kigoma. | Ally M. Adon (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 32. | Lake Oil Limited- Igunga Petrol Station, S. L. P 5055. Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 480, Kitalu "A", Eneo la Chabutwa, Igunga, Tabora. | Ally Edha Awadh (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 33. | Lake Oil Limited-Ujiji, S. L. P 5055, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 67,68 & 69, Eneo la Ujiji, Kigoma. | Ally Edha Awadh (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 34. | Lake Oil Limited Mkamba, S.L.P. 5055, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 14, Kitalu "A", Eneo la Ifakara, Wilaya ya Kilombero, Mkoa wa Morogoro | Ally Edha Awadh (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 35. | Donald Simango Mejiti, S. L. P 2993, Dodoma. | Kijiji cha Mpwayungu, Chamwino, Dodoma. | Donald Simango Mejiti (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 36. | Pahi Filling Station, S.L.P. 23, Kondoa | Kijiji cha Pahi, Kondoa,Dodoma. | Haruna Hassan Mfalla (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 37. | Landmark Filling Station - Kibaigwa, S. L. P 64, Kongwa. | Kiwanja Na. 1, Eneo la Mandela, Kibaigwa, Kongwa,Dodoma. | Fatuma Ramadhani Mganga (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 38. | Puma Energy Tanzania Limited, S. L. P 9043, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 168, Eneo la Msalato, Dodoma. | Fatma Abdallah (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 39. | Njombe Filling Station Company Ltd – Nkuhungu, S. L. P 411, Njombe. | Kiwanja Na. 99, Kitalu B, Eneo la Nkuhungu, Dodoma. | James Malika Mwinuka (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 40. | William Costantino Mhanga T/A Rabbit Filling Station, S. L. P 40898, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "A", Eneo la Dinginayo, Kilolo, Iringa. | William Costantino Mhanga (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 41 | King Fresh Co. Ltd, S. L. P 60, Mafinga. | Eneo la Ikanga, Mdabulo, Mufindi, Iringa. | Zuberi Mkemesa (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 42 | Costa Rashid Ngumbi Igowole, S. L. P 111, Mufindi. | Kiwanja Na. 8, Kitalu "B", Eneo la Igowele Mufindi, Iringa. | Costa Ng'umbi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 43 | Seleman Tullo Mdoe T/A Kwesine Petroleum, S. L. P 45370, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "J", Eneo la ilongeroi, Singida. | Seleman Tullo Mdoe (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 44 | Afroil Investment Limited, S. L. P 38383, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 480, Kitalu "Y", Eneo la Kibaoni, Singida. | Hilmy Ahmed Mbarak (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 45 | M/S Nyamse Petrol Station - Ngulyati, S. L. P 200, Magu. | Kijiji cha Ngulyati, Ngulyati, Bariadi Simiyu. | Hassan Hamis Nyamse (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 46 | Blue Wave Emporium Limited, S. L. P 11624, Mwanza. | Kiwanja Na. 1733, Kitalu "B", Eneo la Igombe, Ilemela, Mwanza | Ephrahim Stanley Fimbo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 47 | Deus Marcel Rwebale T/A Benaco Oil, S. L. P 57, Ngara. | Kiwanja Na. 1068, Kitalu "B", Eneo la Kasulo, Ngara, Kagera. | Deus Marcel Rwebale (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 48 | Gyunda General Supply, S. L. P 89, Ngara. | Kijiji cha Mukikomero, Ngara, Kagera. | Deogratius Nicholauce Kidenke (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 49 | Ongujo Investment Co. Ltd - Kirongwe, S. L. P 75, Rorya - Mara. | Kijiji cha Kirongwe, Bukura Rorya, Mara. | Ongujo Wakibara Nyamarwa (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 50 | Petroafrica (T) Limited-Tambukareli Service Station, S. L. P 4878, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 118, Kitalu "A", Eneo la Tambukareli, Geita. | Yasin Warsame (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 51 | Virian Oil Limited, S.L.P 246, Bunda. | Kiwanja Na. 27 &29, Kitalu "N", Eneo la Bunda, Mara. | Marwa Chogo Marwa (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |

***Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote aliyetajwa hapo juu kwamba asipewe leseni au Kibali cha ujenzi, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.***

Mkurugenzi Mkuu
Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA
41104 Tambukareli S.L.P 2857, Dodoma
Simu: +255-26 2329002-4, Nukushi: +255-26 2329005
Barua-pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: www.ewura.go.tz

Huduma kwa Wateja:0800110030

Imetolewa na:
Mkurugenzi Mkuu
EWURA

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Januari mwezi wenye visingizio kibao

**KILA** inapofika mwezi Januari baadhi ya watu huutumia kama sababu ya kutoa visingizio mbalimbali vikiwamo vya kukosa fedha.

Mwezi Januari ni kama miezi mingine ambayo mtu anatakiwa kujipanga kutimiza malengo yake, lakini baadhi huutumia kuvuruga bajeti zao na kukomba mpaka pesa ya kulipa ada au kodi ya nyumba.

Mwezi huu baadhi ya watu hudhalilika kwa kukopa hata watu ambao hawajawahi kuwakopa na pia husababisha wengine kununia wenzao kwa sababu ya kutopewa walichoomba.

Hata ndugu au jamaa wanapokwenda kuomba msaada kwa wapendwa wao, hujibiwa 'we huoni huu ni mwezi Januari'.

Ni vizuri mwezi huu watu wakajipanga ili kuepuka kukutwa na udhalilishaji wa aina yoyote.

Mwezi huu ulioanza watu wajipange na kuzingatia kujiepusha na magonjwa yasiyoyakuambukiza ambayo ni pamoja na msongo wa mawazo kutokana na kukosa ada na kodi ya nyumba.

Magonjwa yasiyoambukiza ni yale ambayo hayasambazwi kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine kwa kuwa hayana vimelea vinavyohusiana na magonjwa hayo.

Katika nchi zinazoendelea, Tanzania ikiwa mojawapo ajali za barabarani na madhara yatokanayo na vilevi yamewekwa kwenye orodha ya magonjwa yasiyoambukizwa.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), magonjwa yasiyoambukiza ndio yanayoongoza kwa kusababisha vifo duniani.

Utafiti unasema asilimia 72.8 duniani ya vifo vinasababishwa na magonjwa yasiyoambukiza na shinikizo la damu limekuwa kichocheo kikubwa.

Utafiti huo uliofanywa na Nature mwaka 2007 umeripoti kuwa magonjwa yasiyoambukiza yanaua kwa kasi zaidi kulinganisha na yale yanayoambukiza.

Kutokana na takwimu hizo za kidunia kwa hapa nchini katika utafiti uliofanywa mwaka 2012, unaonesha kuwa asilimia 92.6 ya Watanzania ambao vipimo vyao vya shinikizo la damu vina walakini, hawajaanza kutumia dawa, hali inayowafanya kuwa katika hatari ya kupata magonjwa mengine yasiyoambukiza.

Ulaji chakula bila kuzingatia kanuni za afya umeelezwa kuwa chanzo kinachochangia magonjwa hayo kuwakumba watu wengi.

Hivi sasa hospitali nyingi zinapokea wagonjwa wenye magonjwa yanayotokana na tatizo la shinikizo la damu, moyo, figo na mengine ambayo chanzo chake ni mtindo wa maisha wanayoishi.

Wataalam wa afya mara kwa mara wanashauri watu kuzingatia ulaji ulio sahihi na kufanya mazoezi ili kujikinga na maradhi hayo.

Kwa mujibu wa wataalam hao magonjwa yasiyoambukiza yanatumia gharama kubwa kuwatibu wagonjwa kulinganisha na magonjwa mengine.

Magonjwa hayo yanaweza kudhibitiwa kwa watu kufuata kanuni za afya ikiwamo pia kucheki afya zao mara kwa mara ili kujua mwenendo wao.

Kuna wakati mtu anakwenda hospitali kutibiwa tatizo lingine, lakini anapofika na kuangaliwa mwili wake anakutwa na tatizo kubwa.

Utafiti unaeleza kuwa umri wa kuishi kwa wanawake ni miaka 69 na wanaume umepungua kwa sasa wanaishi miaka 62 kwa ajili ya changamoto mbalimbali ikiwamo mabadiliko ya tabianchi, mazingira na mabadiliko katika maendeleo.

Magonjwa yasiyoambukiza imeelezwa kuwa ni changamoto hasa katika umri wa wazee na kila mara kumekuwa kukitolewa elimu kwa kuwashirikisha watu wenye umri huo kuwakumbusha kufanya mazoezi ya viungo ambayo yanasaidia kutoa sumu mwilini na kuimarisha mifupa na nyonga. Moja ya mambo yanayochangia kuongezeka kwa magonjwa hayo ni mabadiliko ya taratibu za kimaisha zinazohusisha matendo yanayoweza kusababisha magonjwa.


Dalili za magonjwa yasiyoambukiza ni watu kujiona kuchoka bila sababu, kichwa kuuma mara kwa mara, macho kutoona vizuria, kushikwa na kizunguzungu mara kwa mara, kutokwa na damu kwenye fisi mara kwa mara, miguu na mikono kuwa na maumivu kama ya kuwaka moto na nyingi zinazofanana na hizo.

Mtu akishaona dalili hizo ni bora akimbilie hospitali na kubadili mtindo wake wa maisha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Walemavu, wazee, yatima, wajane wasikumbukwe kwa sikukuu pekee

**KUMEKUWA** na utaratibu mzuri tu nchini kwetu wa watu binafsi, taasisi mbalimbali na hata wanasiasa kuwakumbuka watu wenye uhitaji wakati wa sikukuu.

Tumekuwa tukiona sikukuu nyingi kama vile Krisimasi, Mwaka mpya, Pasaka, Idd El Fitri, Idd El Hajji, taasisi na watu wengine wakimiminika kutoa misaada mbalimbali ya chakula, nguo, vinywaji, mbuzi, ng'ombe, kuku na vingine vinavyofanana na hivyo.

Watu wenye mahitaji ambao ninawazungumzia hapa ni watoto yatima, wajane, wazee, na hata watu wenye ulemavu ambao kipindi hicho wamekuwa wakipata faraja ya msaada na kutembelewa pia.

Hiki ni kitu kizuri sana kwa sababu kinawafanya wahitaji hao ambao wakati mwingine wanaona kama wametengwa na jamii kujiona kuwa ni sehemu yao.

Mara nyingi yeyote anayeona ametengwa na jamii hukosa kujiamini na wakati mwingine hasa watoto baadaye anaondokea kuwa katili na kufanya mambo yasiyofaa kutokana na kile ambacho anaona kama ni kulipiza kisasi kwani kwenye makuzi yake aliona kama jamii ilikuwa imemtenga.

Watu wanaokwenda kutoa misaada kitu ambacho wanatengeneza kwa wahitaji hao ni kuwapa faraja, kuwafanya kuondokana na mawazo potofu ya kutengwa au kujitenga wenyewe, wakati mwingine kuwafanya waanze kujiamini kwani anaanza kujiona ni watu kama wengine tu.

Kwa siku za karibuni tumeona hata klabu za mpira kama vile Simba, Yanga, Azam, na zingine za ligi kuu zimeanzisha utaratibu huu.

Zikitaka kuanza kucheza Ligi Kuu, yaani kabla ya msimu mfano Simba Day, au Siku ya Mwananchi, hufanya shughuli za kijamii ikiwamo kutembelea wahitaji, wagonjwa mahospitalini na hata kutoa damu.

Hili ni jambo zuri na linapaswa lipongezwe na liendelee kwa watu wote kwani lina faida nyingi ambazo nimezieleza.

Hata hivyo ushauri wangu ni kwamba tusiwaache peke yao mpaka siku za sikukuu tu ndiyo taasisi na watu waanze kufuatana kwenda kutoa misaada na kuwaangalia.

Nadhani sasa Watanzania tuanze kuwa na utamaduni wa kwenda kuwaangalia mara kwa mara, kutoa misaada kula nao chakula na kuwafariji.

Tunaambiwa kwenye dini zote kuwa unapotoa kwa watu wenye uhitaji kama hao kwa asilimia 100, basi unapata thawabu kubwa, hivyo uwepo utamaduni wa mtu mmoja mmoja, familia, au vikundi kuchangishana pesa na kwenda kuwatembelea kuwapa msaada na kuwafariji.

Wahitaji hao wasizoee kuona mpaka ikifika sikukuu ndiyo waanze kuona wageni wakimiminika. Waanze kuzoea kupokea wageni mara kwa mara hata kama siyo siku za sikukuu, na ikifika wakati huo ndiyo waongezeke zaidi.

Kuna vitu vingi vya kujifunza iwapo yeyote atakwenda kuwatembelea wazee, yatima, wajane, wafungwa, hata walemavu, kama ambavyo baadhi wanavyojifunza wakienda kutembelea wagonjwa hospitalini.

Ifanywe kama sehemu ya mtoko, kama vile wanaokwenda baa, klabu, ufukweni au 'pikniki'.

Siku hizi kuna vikundi vingi, vikiwemo vya kusaidiana, kutenga wikiendi moja kwenda kutoa msaada, kushinda na kula na watu wenye mahitaji ni jambo litawafanya kuwa na amani ya moyo.

Niwapongeze Watanzania wote ambao wamekuwa na utamaduni wa kuwasaidia na kuwatembelea nyakati za sikukuu. Ushauri wangu sasa waanze kutembelewa sasa hata siku za kawaida ili wakati mwingine kujua shida zao za kila siku zinazowakabili.

# Meya ataka msamaha matibabu kwa yatima

**Na Mussa Mwangoka,**
MPANDA

MEYA wa Manispaa ya Mpanda mkoani hapa, Haidary Sumry ameomba serikali kutoa msamaha wa matibabu kwa watoto wanaolelewa katika vituo vya yatima ili waondokane na changamoto za kukosa huduma za matibabu katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

Alisema hayo katika hafla ya kula chakula cha mchana na watoto yatima wanaolelewa katika cha malezi cha Kanisa Katoliki kilichoko kata ya Nsemulwa, Manispaa ya Mpanda, huku akikabidhi misaada ya kiutu na bima za afya za matibabu kwa watoto 20.

Alisema matunzo ya watoto ikiwamo kuwasaidia kupata huduma sahihi na bora za afya ni jukumu la wananchi wote, ikiwamo serikali, hivyo ipo haja serikali kuona namna ya kusaidia vituo hivyo kwa kutoa msamaha wa matibabu kwa kundi hilo.

Meya huyo aliongeza kuwa kinachopaswa kufanyika sasa ni ama kuwatengenezea bima maalumu zitakazowawezesha kupata matibabu mazuri na yenye uhakika au kutoa msamaha wa matibabu kwa kundi hilo.


Alisema zipo taarifa kwamba mazingira ya uendeshaji vituo hivyo ni magumu, baadhi ya watoto wamekuwa wanakumbana na vikwazo katika kupata huduma za matibabu.

"Hivi vituo vinasaidia tu kufanya kazi hii. Lilipaswa kuwa jukumu la serikali, hivyo kwa upendo na huruma tumwombe Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan aone uwezekano wa kusaidia vituo hivi kwa kutoa msamaha wa matibabu au bima maalumu zitolewe kwao," alisema.

Meya huyo pia alitoa wito kwa jamii, hususani wanawake ambao kila mwisho wa mwaka wanavunja vikoba na makundi mbalimbali, kutoa sehemu ya kile wanachopata kwa kusaidia makundi maalumu yenye uhitaji.

Awali, Mlezi kiongozi katika kituo hicho, Sista Rose Sungura alisema jamii inapaswa kuelewa kwa ni wajibu wa watu wote kuwalea watoto wenye uhitaji, wakiwamo yatima.

Hivyo, alitoa wito kwa wananchi wa Mpanda kujitokeza na kutoa misaada ya kiutu itakayosaidia kupunguza changamoto katika malezi ya watoto hao.



Ofisa Utumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Singida, Amaniel Samweli, akichangia damu katika hafla iliyofanyika juzi eneo la Soko Kuu la Singida. Uchangiaji huo ulihamasishwa na Amiri George ambaye ilikuwa maadhimisho ya siku yake ya kuzaliwa kwa kuchangia damu yeye na marafiki zake kwa ajili ya Hospitali ya Manispaa ya Siginda. **PICHA:THOBIAS MWANAKATWE**

# 188 wachunguzwa, kutibiwa moyo JKCI

**Na Christina Mwakangale**

MAKUNDI maalum, wakiwamo watu wenye ulemavu 188, wamefanyiwa uchunguzi na kupatiwa matibabu ya magonjwa ya moyo na maradhi yasiyoambukiza kama vile kisukari na presha huku 20 wakipewa rufani.

Matibabu hayo yamefanyika wakati wa hafla fupi ya chakula cha mchana na zawadi kwa makundi hayo iliyoandaliwa na Taasisi ya Mama Ongea na Mwanao katika viwanja vya Karimjee, jijini Dar es Salaam.

Bingwa wa Magonjwa ya Moyo JKCI, Dk. Mohamed Aloyce, alisema katika upimaji huo, watu wenye ulemavu 20 wamepewa rufani kufika katika tawi la taasisi hiyo lililoko Kawe kwa ajili ya matibabu zaidi.

"Tumewakuta baadhi ya watu wana matatizo ya shinikizo la juu la damu, lakini kutokana na vipato vyao kuwa chini wanashindwa kwenda hospitalini kupata matibabu, wengine hata wakienda na kupewa dawa mara moja hawarudi tena," alisema Dk. Aloyce.

Bingwa huyo alisema kuwa kupitia hafla hiyo, watu wenye ulemavu wamepata huduma za afya ingawa bado kuna mahitaji ya wao kuwa na bima ya afya kwa kila mmoja, ili pale wanaopopata changamoto za afya watibiwe kirahisi.

Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Stevene Mengele, alisema taasisi hiyo imewakusanya watu wenye ulemavu na kukaa nao pamoja ili kuwapa faraja.

Stevene alisema kundi la walemavu limesahaulika ndio maana baada ya kuwakusanya wakaona kuna umuhimu wa kupimwa magonjwa ya moyo, kucheza nao na kuwapa faraja ili wajisikie kuwa sawa na wengine.

Stevene aliwapongeza wataalam wa afya kwa kuwa na moyo wa kujitoa kwa watu hao kuhakikisha wote waliohitaji huduma ya uchunguzi wa afya wanapata kwa wakati.

> **"Tumewakuta baadhi ya watu wana shinikizo la juu la damu, lakini kutokana na vipato vyao kuwa chini wanashindwa kwenda hospitalini ...**

"Kazi ya kutibu ni ngumu, Mungu awasimamie. Tunaomba sana msituache hata hapo baadaye tukiwataka tena mtukubalie, ili kwa pamoja tuweze kuwafikia watu wa kundi hili kupata huduma hizi muhimu za afya," alisema Stevene.

Wakizungumza baada ya kupima afya, wanufaika wa huduma hiyo walishukuru serikali kwa kutoa huduma hiyo kwao kwa kuwa wengi wao hawakuwahi kufanya vipimo kama hivyo na hawakuwa na matarajio ya kupima moyo katika maisha yao.

Joseph Jackson, mkazi wa Mbagala, alisema hakujua kama ana tatizo la kisukari hadi alipopima na kupata majibu katika hafla hiyo.

"Ninashukuru sana serikali yangu kwa kutusaidia kupata huduma za afya, leo nimepima magonjwa ya moyo, sukari, na shinikizo la damu na kukutwa na tatizo la sukari.

Nimepewa rufani na nina ahadi kwenda kuchunguza zaidi," alisema.


Agnes Mwanuke, mkazi wa Temeke, alishukuru JKCI kwa kutoa huduma za uchunguzi na matibabu ya magonjwa ya moyo kwa watu wenye ulemavu kwa kuwa amekuwa akipata maumivu makali upande wa kushoto wa moyo lakini kutokana na utafutaji wake kuwa mgumu, hakufikiria kwenda hospitalini kutibiwa.

"Sisi watu wenye ulemavu utafutaji wetu ni wa shida sana, hivyo kushindwa kupata kipato cha kutupeleka hospitalini kupata huduma za matibabu, lakini walivyotusogezea hapa tunawashukuru sana kwa kuwa tumechunguza afya zetu," alisema Agnes.

Aliomba huduma hizo zisiishie kwao tu, bali taasisi hiyo iangalie pia namna ya kuwafikia wenye ulemavu wengine nchini ili nao wapime afya zao kwa kuwa afya ndio mtaji wa maisha.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# Jussa, wanachama ACT wasema Othman anatosha urais Zanzibar

**Rahma Suleiman na Joyce Lameck**

SIKU moja baada ya Mwenyekiti wa Taifa wa ACT-Wazalendo Taifa, Othman Masoud Othman, kutangaza nia ya kugombea urais wa Zanzibar, baadhi ya viongozi wa chama hicho wamesema "anatosha".

Waliosema Othman ana sifa za kupeperusha bendera ya ACT-Wazalendo kwenye Uchaguzi Mkuu uliopangwa kufanyika Oktoba mwaka huu, wametaja sifa ya uzoefu na uadilifu kama nyenzo itakayokipa chama hicho ushindi.

Othman ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, alitangaza nia ya kugombea urais visiwani humo juzi alipozungumza na wahariri mjini Unguja katika salamu zake za Mwaka Mpya 2025.

Katibu Mkuu wa Baraza Kivuli la ACT-Wazalendo, Seif Hamad Suleiman, alisema Othman ni mtu sahihi kwa wakati sahihi kwa sababu historia yake kwenye utumishi wa umma ni nzuri.

Alisema Othman ametumikia Serikali ya Zanzibar kwa zaidi ya miaka 30 na kuteuliwa nyadhifa mbalimbali, ikiwamo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na hajawahi kuwa na kashfa.

Alisema Othman ana uwezo mkubwa kiutendaji, hivyo anaweza kuivusha Zanzibar kuwa na maendeleo zaidi.

Mjumbe wa Baraza Kuu wa chama hicho, Ismail Jussa Ladhu, alisema Othman ni mtu sahihi na chama kinamwamini kwa sababu hana tabia ya kupindisha maneno na kwamba ni mtu mwenye msimamo imara.

Alisema Othman ana sifa zote zinazohitajika na ana vigezo vya kuwa mgombea urais wa Zanzibar na wakati utakapofika chama kitamuunga mkono.

Katibu wa Idara ya Habari ACT-Wazalendo, Salum Bimani alimpongeza Othman kwa kutangaza nia hiyo mapema.

Alisema ana imani na kiongozi huyo kuwa anao uwezo wa kuwania nafasi hiyo kwa kuwa ni kiongozi mzuri na anastahili kupeperusha bendera ya ACT-Wazalendo Oktoba mwaka huu.

"Siamini kama kuna mtu anaweza kuchukua fomu kwa mapenzi yake ili kushindana na Othman katika viwango vyake vyote kitaifa na kimataifa, ni mgombea anayeuzika na kununulika pia, ni bidhaa nzuri na yenye soko kwa uchaguzi wa Oktoba 2025," alisema Bimani.

Mmoja wa wanachama wa chama hicho, Hassan Njani, alisema ni vizuri kiongozi kujitangaza mapema ili kuwapa wananchi nafasi katika kuamua kama atafaa katika kuongoza.

"Unapojitangaza mapema kuwania nafasi, wananchi wanapata muda mzuri wa kutafakari juu ya uadilifu wako katika maisha ya siasa, ili kukupima na kukutambua una vigezo vyote ambavyo vinafaa kuwa kiongozi hasa kwa nafasi hiyo juu ya uongozi wa serikali," alisema.

Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. George Kahangwa, akizungumzia suala hilo, alisema ni haki ya kiongozi kutia nia mapema kwa kuwa inampa nafasi ya kujiandaa kwa ajili ya kuwa kiongozi mzuri.

Pia inasaidia wananchi kufanya uamuzi sahihi katika kumchagua kiongozi sahihi na mwenye kutekeleza majukumu yake kwa uadilifu na kumtambua kama aweza kuwa kiongozi kwao.

Othman ametangaza kuwania urais wa Zanzibar akitaja kusimamia mambo 11, aliyosema yatavipaisha visiwa hivyo kimaendeleo, akiyataja yanajumuisha kujenga ustawi wa uchumi, kurejeshea wananchi haki ya kuwawajibisha viongozi na kujenga misingi ya utawala bora.

Pia alitangaza msimamo wa chama chake kwamba kitashiriki Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, bila kujali hali ya kisiasa iliyopo nchini.



Mwenyekiti wa jumuiya ya wazazi wa CCM wilaya ya Babati mjini, Emmanuel Khambay (kulia) akipongezwa na Shekhe wa mkoa wa Manyara, Muhammad Kadidi, baada ya kutoa msaada wa vitanda 18 na magodoro 33 vyenye uwezo wa kulaza wanafunzi 36 wa Chuo cha Mahaad Hayat Islamiya, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Vifaa vilivyoibwa Tanesco, TRC DAWASA, vyakutwa kiwandani

**Na Julieth Mkireri,**
MKURANGA

SERIKALI mkoani Pwani imekamata shehena ya miundombinu ya serikali iliyoibwa na kuhifadhiwa katika kiwanda cha kutengeneza vifaa vya ujenzi kilichopo Mkuranga, mkoani Pwani.

Miundombinu hiyo imekamatwa baada ya kuundwa kikosi kazi maalumu kilichoundwa na mkoa huo kwa ajili ya kufuatilia uharibifu wa miundombinu uliokuwa ukifanyika katika taasisi mbalimbali ikiwamo Tanesco.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, ameongozana na viongozi mbalimbali wa mkoa huo na Wilaya ya Mkuranga kukagua miundombinu hiyo ambayo imebainika kuwa ni ya Tanesco, Dawasa na Shirika la Reli (TRC).

Akizungumza na waandishi wa habari katika kiwanda cha LN Features kilichopo Mkuranga ilipokutwa miundombinu hiyo, Kunenge alisema wapo wananchi wanaisaliti serikali na kuhujumu miundombinu inayosambaza huduma.

Kunenge alisema serikali inafanya jitihada ya kuboresha miundombinu, lakini bado wapo wachache wanaohujumu na kurudisha nyuma maendeleo kwa kufanya uharibifu.

"Hatutavumilia yeyote atakayehusika kurudisha nyuma maendeleo ya serikali tutafuatilia tujue nani anayehusika katika hili," alisema Kunenge.

Alisema kwamba pamoja na mkoa huo kuongoza katika uwekezaji wa viwanda, hawataruhusu kuwa na wawekezaji wanaohusika kurudisha nyuma jitihada za serikali.

Kamanda wa Polisi mkoa wa kipolisi Rufiji, Protus Mutayoba, amesema miundombinu hiyo imeibwa katika maeneo mbalimbali na kupelekwa katika kiwanda hicho.

Kamanda Mutayoba amemuomba Mkuu wa Mkoa wa Pwani operesheni kama hiyo kufanyika maeneo mingine ili kukomesha biashara hiyo.

Alisema katika mkoa huo operesheni ya miundombinu hiyo ilianza Novemba 21 na inaendelea, watuhumiwa mbalimbali wamekamatwa na wengine tayari wamefikishwa mahakamani.

Meneja wa Huduma za Usalama Tanesco, Lenin Kiobya alisema kutokana na kukua kwa biashara ya kopa kumesababisha miundombinu mingi ya Shirika la Umeme kuharibiwa kwenye transfoma.

Alisema kwa kipindi cha mwezi Juni hadi Desemba 2023, transfoma 33 zimeharibiwa kati ya hizo 21 ni za maeneo ya Wilaya ya Mkuranga na zilizosalia ni katika maeneo mengine.

Kiobya alisema biashara ya kopa imepanda kutoka Sh. 10,000 kwa kilogramu moja hadi Sh. 30,000 na maeneo ya mpakani mwa nchi imefikia hadi Sh. 100,000 jambo ambalo limesababisha kushamiri kwa biashara hiyo.

Alibainisha kwamba tangu kufanyika kwa operesheni hiyo uharibifu wa transfoma umepungua baada ya kutokuwapo taarifa.

Aliomba kuwapo na sheria ya kuzuia wafanyabiashara kununua miundombinu ya serikali ili kusaidia kukomesha biashara hiyo na uharibifu ambao unafifisha huduma kwa wananchi.

Miundombinu iliyokamatwa katika kiwanda hicho ni pamoja na nyaya za transfoma, vipuri vinavyotumiwa na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), miundombinu ya TRC, TTCL na kopa za Tanesco.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# TRA kuwapa elimu ya kodi viongozi wa dini nchini

**Na Halfani Chusi**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imesema inakusudia kutoa elimu ya kodi kwa viongozi wa madhehebu yote ya dini nchini ili nao wakaitoe kwa waumini wao watambue umuhimu wa kulipa kodi.

Jana mkoni Dar es Salaam, Kamishna Mkuu wa TRA, Yusuph Mwenda alisema hayo alipokutana na Muft na Shekhe Mkuu wa Tanzania, Dk. Abubakar Zubeir katika ofisi za Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) zilizoko Kinondoni.

Akiwa ofisini huko, Kamishna Mkuu alimpongeza kiongozi huyo kwa kutoa elimu ya kodi kwa waumini na kulipa kodi vizuri kupitia taasisi zao nyingine.

Alisema BAKTWA licha ya kuwa ni taasisi ya kidini, ina shughuli inazofanya zinazoifanya ilipe kodi.

"Tunachokifanya kwa BAKWATA, tutakifanya kwa taasisi nyingine kwa sababu kulipa kodi ni ibada na taasisi za kidini zinahamasisha ulipaji kodi.

"Waumini wa taasisi za kidini wamewajibika kulipa kodi na tunaahidi kutenda haki kwa watu wote, anayestahili atalipa asiyestahili hatutamwonea," alisisitiza Kamishna Mwenda.

Alisema TRA inaamini kwa kutumia majukwaa ya kidini kufikisha elimu ya kodi kwa jamii, kutaleta manufaa kwa kuwa viongozi wa dini wana watu wengi wanaowasikiliza.

"Faida za kodi zipo nyingi sana, leo watu wanatibiwa, ni kodi; watoto wanasoma, ni kodi, nchi inajengwa, ni kodi," alisema Kamishna Mwenda.

Kufanikisha suala la utoaji elimu hiyo, alisema timu ya wataalamu wake na BAKWATA watatengeneza mpangokazi na mara utakapokamilika, kazi itaanza.

Muft na Shekhe Mkuu wa Tanzania, Dk. Zubeir alishukuru mamlaka hiyo kwa kufika ofisini kwao kuwapongeza na kuzungumza kuhusu namna ya kutanua wigo wa ulipaji kodi.

Alisisitiza umuhimu wa mamlaka hiyo kutoa elimu kwa viongozi wa dini, kwamba itawajenga vizuri wakati wanawaeleza waumini wao.

Na Ha
MA
Tanza
inaku
ya ko
madh
nchin
waum
umuh
Jan
Salaa



# Rais Samia, viongozi waombewa dua

Na Hamida Kamchalla, TANGA

VIONGOZI wa dini, wakazi wa Mkoa wa Tanga wameungana na mkuu wao wa Mkoa, Dk. Batilda Buriani kuliombea dua taifa, Rais Samia Suluhu na viongozi wengine kudumisha amani nchini na kuondoa mabalaa.

Maombi hayo yalifanyika jana katika viwanja vya urithi ikiwa ni sehemu ya Tamasha la Tanga Urithi kwa ajili ya kutangaza fursa za utalii mkoani hapa, tamaduni za watu wa Tanga na kuwarithisha vijana tamaduni za watu wa pwani.

Mwenyekiti wa Kamati ya Amani Mkoa wa Tanga, Shekhe Jumaa Luwuchu, alisema maombi hayo ni kumshukuru Mungu kwa kuwapatia neema ya kuwa na viongozi mahiri na waadilifu nchini.

"Tunamshukuru Mungu kwa kutupatia kiongozi Rais Samia ambaye ni msikivu, mpole mwenye imani na mstahimilivu, tunaomba aendelee kumlinda azidi kutufanyia mazuri hapa nchini," alisema.

Alisema maombi hayo vilevile yamejikita kumuomba Mungu aendelee kuilinda nchi idumu katika umoja na amani kipindi hiki kuelekea Uchaguzi Mkuu, Oktoba mwaka huu.

**"Tunamuombea kwa Mungu, mkuu wetu wa mkoa kwa namna anavyojitoa kutuletea maendeleo, ajaalie ustahamilivu na afya njema aendelee kuwatumikia Wanatanga vizuri, "alisema Shekhe**

"Tunamuombea kwa Mungu, mkuu wetu wa mkoa kwa namna anavyojitoa kutuletea maendeleo, ajaalie ustahamilivu na afya njema aendelee kuwatumikia Wanatanga vizuri, "alisema Shekhe Luwuchu.

Mchungaji wa Kanisa la Sabato Tanga, Endrew Mdeme, alisema amani ndio msingi wa maendeleo yote duniani.

"Kwa dua hii tutaendelea kumuomba Mungu aweze kuwalinda viongozi wetu katika kufanya maamuzi ambayo yataweza kuleta baraka katika nchi yetu," alisema Askofu Mdeme.

Kwa upande wake Dk. Batilda, alisema Serikali imefanya maendeleo makubwa kwa Tanga kwenye sekta za elimu, uchumi na afya .

Alisema kwa Bandari ya Tanga, maboresho yaliyofanywa yamesaidia ndani ya kipindi cha miezi mitano kupokea meli takribani 172 na kushusha shehena ya mizigo kwa siku tatu.

"Tunamshukuru Rais Samia kwa maboresho makubwa ya miradi ya kimkakati ambayo imeweza kusaidia kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi," alisema mkuu huyo wa mkoa.



Watoto wakibembea na kuogelea katika viwanja vya Msekwa Park wilayani Muheza Tanga kusheherekea Mwaka Mpya juzi.
**PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mfugaji ajimaliza kwa kitanzi

Na Allan Isack, KITETO

MFUGAJI wa Kijiji cha Kimana wilayani hapa Mkoa wa Manyara, Happy Memiruti (38), amefariki dunia kwa kudaiwa kujinyonga na kamba ya kufungia ng'ombe kwenye paa la nyumba.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Manyara, Ahmed Makarani, alisema tukio hilo lilitokea juzi nyumbani kwa mfugaji huyo

Makarani, alisema chanzo cha mfugaji huyo kujiua, hakijafahamika, polisi wanaendelea kufanya uchunguzi.

Awali, alisema mfugaji huyo, alijiua kwa kujinyonga kwa kujitundika kwa kamba ya kufungia ng'ombe aliyoifunga kwenye paa la nyumba yake.

Alisema mwili wa marehemu huyo, umehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Kiteto. Mmoja kati ya majirani wa marehemu, Neema Sinjori, alisema wamesikitishwa na uamuzi wa mwenzao huyo kufa kwa kujinyonga. "Hatujui ni ukatili amefanyiwa au kuna manyanyaso yamefanyika, tumepigwa na butwaa kwa kutotambua kiini cha mwanamke huyo kujinyonga kwa kutumia kamba," alisema.

Kaka wa marehemu huyo, Marengoni Saibulu, alisema mdogo wake, alikuwa mpole , hakupenda kufanya vurugu na mtu yeyote, kitendo hicho kimewashangaza mno.

"Ni mtu ambaye alikuwa mpole hakuwa na kelele na mtu wakiwemo majirani zake au nyumbani kwake, hivyo tumeshangazwa na tukio hilo," alisema Marengoni.

Mume wa marehemu huyo, alisema siku ya tukio hilo, hakukuwa na tatizo lolote kwa kuwa walikunywa chai pamoja na watoto kisha akaondoka nyumbani.

"Nilikwenda kwa ndugu yangu kuongea naye kidogo mara nikapewa taarifa kupitia jirani kuwa nyumba ya mke wangu imefungwa kwa ndani kurudi nikakuta hali hiyo," alisema.

Alisema mke mdogo na jirani baada ya kuchungulia dirishani, waliona mwili wake ukining'inia na kutoa taarifa kwa viongozi wa kijiji na polisi, wakafika na kuvunja mlango.

# Watoto 31,000 wapata lishe bora

Na Allan Isack, NGORONGORO

WATOTO wanaokadiriwa kufikia 31,000 wilayani hapa Mkoa wa Arusha wana hali nzuri ya lishe, imefahamika.

Takwimu hizo zimo katika Tathimini ya lishe iliyofanyika wilayani hapa kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka kuanzia Julai hadi Septemba mwaka jana,

Takwimu hizo zilitolewa kwenye kikao kilichofanyika hivi karibuni, kikiongozwa na Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya hiyo, Boniface Lugola.

Lugola, alisema hali ya lishe kwa watoto ambao ni sawa na asilimia 92.81 imeendelea kuimarika kutokana na kupata lishe bora.

Aliwapongeza wataalamu wa lishe na wadau wa afya wilayani hapa kwa kudumisha hali nzuri ya afya na lishe kwa watoto.

"Tunawapongeza maofisa lishe, watendaji wa kata na wataalamu wengine kwa kuwa mmefanya kazi kubwa, hivyo tuendelee kufanya kazi ili kutokomeza kabisa hali mbaya ya lishe kwa watoto wilayani kwetu," alisema Lugola, ambaye ni Ofisa Tawala wa Wilaya hiyo .

Alitoa rai kwa wajumbe wa afya wilayani hapa kuendelea kusimamia shughuli za lishe katika jamii kuanzia shuleni, nyumbani na kuhimiza upandaji miti ya matunda kama sehemu ya kampeni ya kuboresha afya za watoto na watu wazima.

"Licha yakuwa tuna viashiria vizuri vya hali ya lishe, naomba tuchukue hili kama azimio, sisi wajumbe tuhakikishe miti ya matunda inapandwa katika shule zetu ya kutosha," alisisitiza Lugola.


Akisoma taarifa ya utekelezaji wa shughuli za lishe kwa kipindi cha Julai hadi Septemba mwaka jana, Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Angela Mbaga, alisema watoto 33,337 walifanyiwa tathmini ya hali ya lishe.

Kwa mujibu wa Angela, kati ya hao, 30,940 sawa na asilimia 92.81 walikutwa na hali nzuri ya lishe na asilimia 6.95 sawa na watoto 2, 317 hali mbaya ya lishe.

Alisema kwa kipindi cha miezi mitatu walifanya Maadhimisho ya Siku ya Afya na Lishe katika kata saba kati ya 28 za halmashauri hiyo.

Alizitaja kata zilizofanyiwa maadhimisho hayo kuwa ni Maalon, Ololosokwan, Oloipiri, Kirangi, Orgosorock, Enguserosambu na Olorien Magaiduru.

Angela, alisema wakati wa maadhimisho hayo walitoa huduma za Kliniki ya MKOBA, upimaji wa hali ya lishe kwa watu wazima na kutoa ushauri nasaha kuhusu lishe bora. Alisema akina mama 12,156 kati ya 12,511 walipatiwa vidonge vya madini chuma ili kuboresha afya kwa wajawazito, elimu ya lishe ya makundi ya chakula, uandaaji wa mlo kamili na chakula cha nyongeza kwa watoto wadogo.



# Polisi wawageuzia kibao wamiliki mabasi mikoani

**Na Restuta Damian,** KAGERA

JESHI la Polisi Mkoa wa Kagera, limetangaza msako wa wamiliki wa mabasi kwa kosa la kuendeshwa kwa mazoea na dereva mmoja na kuchangia ongezeko la ajali barabarani mkoani hapa.

Msako huo umetangazwa na Kamanda wake, Blasius Chatanda wakati akizungumzia hatua wanazochukua ili kubaliana na ajali hizo kwa kipindi cha mwaka huu.

Chatanda, alisema wataanza kuwachukulia hatua kali wamiliki wa mabasi hayo ya abiria yanayofanya safari ndani na nje ya mkoa wao ili kukabiliana na uendeshwaji huo wa mazoea.

Alisema wamiliki wanatakiwa kuhakikisha kwenye mabasi yao, kunakuwa na madereva wawili, kwa mujibu wa sheria za usalama barabarani ili kudhibiti ajali.

Alisema madereva hao, mmoja anapoanza safari na kuchoka katikati, anasaidiwa na mwenzake kwa kumpokea hadi mwisho wao wa safari.

"Tumeshasisitiza maderava wawili kama mabasi yanafanya safari ndefu kuanzia saa nane njia, zikiwemo za Bukoba (Mkoa wa Kagera) kwenda Dar es Salaam na nyingine, lakini bado utakuta wanafanya kazi kwa mazoea hali inayopunguza umakini barabarani," alisema Chatanda.

**Mmoja wa kinamama waliojifungua usiku huo, Vicky Sebastian, mkazi wa Kijiji cha Mogabili, alisema alifika hospitalini hapo majira ya saa 4:00 asubuhi Desemba 23, 2024 na kupewa kitanda**

Alisema wamebaini kuwa huo ni mchezo mchafu wa wamiliki hao baada ya kufanya ukaguzi kwenye mabasi yao kabla ya kuanza safari na katikati ya safari.

Kamanda huyo, alisema wakati wa ukaguzi wa mabasi hayo wanaonekana madereva wawili, likifika katikati ya safari, anakuwa mmoja na hajulikani mwingine alikoteremka.

Chatanda, alisema haiwezekani dereva mmoja atoke na basi mwanzo hadi mwisho wa safari hajapokezana na mwenzake kwani lazima atachoka na kuhitaji msaada. Alisema utaratibu wa basi kuwa na madereva wawili ni suala linalotakiwa lifanywe na wamiliki.

Alisema basi kuwa na madereva wawili, mmoja akipata tatizo ikiwemo kuchoka, atamkabidhi mwenzake kuendelea na safari na kuepuka ajali.

"Kwa kumbukumbu za haraka disemba (mwaka jana) tumepata ajali kwenye maeneo mbalimbali ndani ya mkoa wetu. Wilayani Karagwe ilitokea ajali na kuua watu saba, majeruhi 13 na Biharamulo iliuawa watu 11 na majeruhi 16," alisema Chatanda

Alisema vilevile wamebaini ajali nyingine zimesababishwa na baadhi ya madereva kwa ulevi na wengine kuharibu mfumo wa magari kwa kuendesha kwa mwendo mkali baada ya kuvuka vizuizi vya askari wa kikosi cha usalama barabarani.

Hata hivyo, alisema katika ukaguzi wa mabasi uliofanyika Disemba mwaka jana na wamewakamata madereva tisa na kuwanyanga'nya leseni.



Wazazi kutoka Mtaa wa Nganza, kata ya Luchelele jijini Mwanza, wakifurahia jambo wakati wakiwalisha chakula watoto wao baada ya kupokea elimu ya lishe na uchangamshi kwa mtoto na kisha kuandaa chakula cha asili chenye virutubishi vinavyohitajika kwa mtoto kwa ajili ya maendeleo ya mtoto, elimu inayotolewa na Halmashauri ya jiji kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo.**PICHA:VITUS AUDAX**

## Wananchi wahakikishiwa ulinzi, usalama

**Na Judith Julius,** NGARA

SERIKALI wilayani hapa Mkoa wa Kagera imewahakikishia wananchi wake ulinzi na usalama wa mali zao katika kipindi cha mwaka huu.

Hayo yamo katika taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Ngara, Mathias Julius aliyoitoa juzi.

Julius ambaye ni Mkuu wa Wilaya hiyo, katika taarifa yake, alisema vyombo vya usalama vimejipanga kuhakikisha ulinzi na usalama vinaimarishwa ili kudumisha amani wilayani hapa.

Alisema Jeshi la Polisi wilayani hapa, limepanga askari wa doria maeneo mbalimbali kudhibiti viashiria vya uhalifu wakati wote.

Aliwaomba wananchi kulipa ushirikiano jeshi hilo kwa kutoa taarifa za matukio yanayoweza kuhatarisha usalama wao na mali zao.

Kwa upande mwingine, aliwakumbusha madereva wa bodaboda kuzingatia sheria za barabarani na uendeshaji usiohatarisha maisha ya wengine.

# Mutafungwa: Uhalifu umepungua Mwanza

**Na Vitus Audax,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani hapa limesema uhalifu umepungua kwa asilimia 13 kwa Disemba, mwaka jana ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka juzi.

Hayo yalibainishwa juzi na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Wilbroad Mutafungwa wakati akizungumzia tathimini ya utendaji kazi wa jeshi hilo kwa kipindi hicho mwaka jana.

Mutafungwa, alisema kupitia doria na misako inayoendelea, wamekamata makosa 2,525 na watuhumiwa 3,510 wa makosa ya jinai. Vilevile, alisema wamekamata makosa hatarishi 15,307 ya usalama barabarani na watuhumiwa 14,851, tofauti na kipindi kama hicho mwaka juzi.

Alisema mwaka juzi, watuhumiwa 2,215 wa makosa ya jinai na 13,329 wa makosa hatarishi ya usalama barabarani, walikamatwa ikiwa ni sawa na ongezeko la watuhumiwa 1,295 wa makosa ya jinai na watuhumiwa 1,522 wa makosa hatarishi ya usalama barabarini.

Kamanda huyo, alisema watuhumiwa wa makosa ya jinai walikamatwa kwa kupatikana na mali zinazodhaniwa kuwa za wizi, kucheza kamari, wizi, mauaji, ubakaji na ulawiti na ukahaba.

Alisema jeshi hilo limeimarisha mifumo ya kiusalama kwa kuweka mpango kazi thabiti uliohusisha kupanga askari maeneo mbalimbali kuhakikisha wahalifu hawapati mwanya wa kufanya matukio ya uhalifu.

Kwa upande wa usalama barabarani, alisema makosa 15,307 yamekamatwa kwa kipindi cha Disemba Mosi hadi 30, mwaka jana, madereva 16 kufungiwa leseni kwa kipindi cha miezi sita ikilinganishwa na makosa 13,921 yaliyokamatwa kwa kipindi kama hicho kwa mwaka juzi.

Alivishukuru vyombo vya habari kwa ushirikiana katika kuibua na kudhibiti uhalifu na wahalifu katika kipindi cha mwaja jana.

"Tumefanya kazi kwa pamoja na kwa kiasi kikubwa tumefanikiwa kwa mkoa wetu kuendelea kuwa salama kwa kuwa na ushirikiano madhubuti miongoni mwetu," alisema.

Alisema kwa sasa hali ya ulinzi na usalama katika mkoa huo ni shwari na kwamba wameendelea kuimarisha ulinzi maeneo yote na kuchukua hatua kwa watakaobainika kujihusisha na uhalifu.




Ukurasa 13

Mapaparazi tuombeane Heri ya Mwaka mpya, lakini...!



**AKIVITAJA 15 VIKUBWA VIKO JIKONI... Dk. Samia anavyosafiri na Awamu ya Sita kuhuisha zama za 'Tanzania ya Viwanda'**

Ukurasa 12

BUFE
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
IJUMAA JANUARI 3, 2025
Nipashe

# Serikali katika mapinduzi maendeleo, kupitia ubunifu wa teknolojia za vijana

## • Biteko, Mkenda, bosi COSTECH wafunguka nafasi zao

**Na Renatha Msungu, Dodoma**

TUME ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), ina majukumu ya kitaifa kusaidia wabunifu na watafiti nchini hususani wanaochipukia, wachangie hatua za maendeleo kitaifa katika eneo hilo, wao na nchi kutambulika kitaifa na kimataifa.

Moja ya eneo linalochukuliwa nalo, ni kupitia makongamano ya wabunifu na watafiti kwa nyakati tofauti, hata kuchochea ushawishi wa vijana kuwasilisha mawazo yao ya kibunifu, ili yaboreshwe na kutambulika ndani na nje ya nchi.

Makongamano hayo yamekuwa kichocheo kikubwa kwa wabunifu kupanua wigo na fikra za teknolojia za kisasa, hata wanatatua changamoto za kimaendeleo, hususani kwenye miradi inayotekelezwa katika maeneo tofauti.

Hivi karibuni kulikuwapo kongamano lililoshirikisha wabunifu na watafiti kutoka maeneo mbalimbali nchini, katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere uliopo Dar es Salaam.

Mfunguzi wa kongamano, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Dk. Doto Biteko, akalenga zaidi kuwatambua watafiti waliofanya vizuri kwenye tafiti zao ndani na nje ya nchi.

Hapo yupo Angelina Silvester, mbunifu na mwanzilishi wa Kiwanda cha Kutengeneza mvinyo kwa kutumia zao la nyanya.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Doto Biteko, akimsikiliza mbunifu wakati wa ufunguzi wa Kongamano la Tisa la Sayansi, Teknolojia na Ubunifu. Kushoto kwake ni Mkurugenzi wa COSTECH Dk. Amos Nungu na kulia ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia,. Profesa Adolf Mkenda. **PICHA: RENATHA MSUNGU.**

Hapo anasafiri na hoja ya mikakati hiyo, akisema imekuwa msaada mkubwa unaowanyanyua wabunifu, ili kazi zao zitambulike ndani ya jamii na nje.

Kutokana na hilo, Mtafiti huyo anasema, vijana wenye mawazo chanya ya kubuni teknolojia yoyote, kwa ajili ya kuleta maendeleo wasibweteke na mawazo yao, bali wayawasilishe COSTECH ili yaweze kufanyiwa kazi na kuleta matokeo kwao na taifa kwa ujumla.

Anashauri kuwa, mtu akiwa na wazo lake aanze kwanza kulifanyia kazi na baadaye awasilishe katika sehemu husika kiserikali, ili liboreshwe kwa kuleta matokeo chanya kijamii, pia kusaidia kuimuinua kiuchumi mbunifu.

"Nawashukuru sana COSTECH kutokana na fedha walizonipa kuendeleza teknolojia yangu ya kutengeneza 'wine' kwa kutumia zao la nyanya,"anatamka Angelina.

**DK AMOS NUNGU**

Dk. Amos Nungu, Mkurugenzi wa COSTECH, anasifu kongamano husika inaonesha Tanzania inaendeleza jitihada za kukuza utafiti wa kisayansi, maendeleo ya kiteknolojia na ubunifu, kama msingi wa maendeleo endelevu kiuchumi.

Anataja serikali imefadhili miradi kadhaa katika nyanja mbalimbali za utafiti, zikiwamo kilimo kupitia teknolojia za kisasa za kuongeza tija katika uzalishaji wa chakula, afya kwa ubunifu wa tiba za magonjwa sugu na teknolojia za uchunguzi, ili kutoa suluhisho la utatuzi wa changamoto za kimaendeleo.

Mkurugenzi Dk Nungu, anaeleza kwamba, uwekezaji huo unalenga kuwapa wanasayansi nyenzo na miundombinu inayohitajika, ili kufanikisha ubunifu unaobadilisha maisha ya Watanzania, wakiwamo vijana watakaochangamka kutumia changamoto, kuzigeuza fursa.

Anasema ni mafanikio yanayoonekana, kutokana na ruzuku hizo zinazoleta matokeo chanya, ikiwamo kuongezeka utafiti wa kisayansi, ambayo kwa kiasi, inafungua nafasi za ajira hasa kwa vijana, pia fursa kwa watafiti na wabunifu vijana.

Anasema, katika kushirikisha jamii, miradi mingi imejikita kuwahusisha wananchi moja kwa moja, kuhakikisha matokeo yanawiana na mahitaji halisi ya jamii.

**WAZIRI WA ELIMU**

Profesa Aldolf Mkenda, Waziri

Inaendelea Uk 14

BIASHARA

AKIVITAJA 15 VIKUBWA VIKO JIKONI...

# Dk. Samia anavyosafiri na Awamu ya Sita kuhuisha zama za 'Tanzania ya Viwanda'

- Awakutanisha Bashe, Jafo waje na jibu la sukari nchini
- Mnamo 2021, Dk. Mpango alidokeza usakaji viwanda

**Na Mwandishi Wetu**

JANA gazeti hili lilikuwa na uchambuzi unaohusu hatua na nyendo za Serikali ya Awamu ya Sita kimaendeleo, ikiangaziwa mwenendo, utekelezaji, uwekezaji katika afya, pia dira yake.

Maudhui yake mahsusi, yanaangazia afya ya mwanamke na mtoto, ambayo ndiyo ajenda muhimu nchini na duniani.

Lakini katika sura ya pili, kuna ngazi ya maendeleo, ambayo nyenzo mojawapo ni kupitia uchumi, ambao sekta ya viwanda kitaifa ni eneo muhimu sana.

Miaka mitatu iliyopita, Dk. Philip Mpango, Makamu wa Rais katika Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akaitolea ufafanuzi, akiwa na maelezo kwa niaba ya mkuu wa nchi akisema:

"Sekta ya viwanda ndio chimbuko la maendeleo ya haraka ya nchi mbalimbali na mhimili mkuu wa kutegemewa katika kuongeza thamani ya malighafi tulizo nazo, kutoa ajira kwa wananchi,"

Dk. Mpango akaendelea kutaja mengine: "...na kuongeza mapato ya serikali, pamoja na fedha za kigeni na kuongeza kuboresha sayansi na teknolojia."

Ilikuwa katika tukio lililofanyika Oktoba mwaka 2021 ikiwa ni hafla ya kutoa Tuzo za Rais kwa Wazalishaji Bora wa Viwanda nchini iliyoandaliwa na Shirikisho la Viwanda Tanzania (CTI) kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara jijini Dar es Salaam.

Akasisitiza msimamo wa Sekta ya Viwanda katika zama Awamu ya Sita ya Rais Dk. Samia, ina jukumu la kuhakikisha nchi inapenya katika soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na lile la Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC),

Dk. Mpango akasisitiza haja ya kuhakikisha kunakuwapo uuzaji bidhaa katika soko la EAC unaongezeka kufika asilimia 15 kwa hatua ya wakati huo, lengo ni asilimia 30 wa soko lote. Ilikofika ilikuwa asilimia saba.

Akataka namna mojawapo akiitaja ni: "Kupenda kununua bidhaa za nje kuna madhara makubwa kwenye ukuaji wa viwanda vyetu, kwa kuwa inasaidia viwanda vya nje viendelee kukua pia kuhamisha ajira kutoka nchini kwetu kwenda nchi za wenzetu"

**KUTOKA KWA RAIS**

NI wiki hii, katika kuukaribisha Rais Dk. Samia akatimiza malengo yake kwa vitendo, alipofahamisha sehemu ya mavuno ya azma yake, akisema viwanda vipya vikubwa 15 viko 'jikoni' vinajengwa.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Kuunganisha Malori na Matipa, Chirag Panna, Kigamboni, Dar es Salaam, alipokagua kazi zake nchini. Mei, mwaka jana.

Hiyo inatamkwa na Rais, huku katika chombo cha habari na Ofisa wa Tume ya Uwekezaji (TIC), kwamba mwaka jana juhudi za Rais Dk. Samia imeweka rekodi, kwani kumesajiliwa miradi wastani 900, ikivuka rekodi kubwa ya awali ya miradi 500.

Mnamo Agosti mwaka huu, Rais Dk. Samia, akawaagiza Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe na Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo kuanza mchakato wa mabadiliko ya sera ili viwanda vya sukari vya ndani viwe na uwezo wa kuzalisha sukari ya viwandani na malighafi ya kuzalisha nishati safi ya kupikia na matumizi mengine.

Hapo akafafanua ni hatua ya kupunguza pengo la upatikanaji sukari nchini, kwani mahitaji ya sukari nchini ni tani 650,000 huku viwandani ni tani 250,000, akisistiza kuendelea kuagiza bidhaa hiyo nje ya nchi ni matumizi mabaya ya fedha za kigeni.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akitangazia wakazi wa mkoa Morogoro serikali inavyojipanga kurejesha hadhi yake kuwa Mkoa wa wa Viwanda, kama ilivyokuwa awali. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Pia, ndani ya mtazamo huo, akawa na ufafanuzi kwamba, dhamira ya serikali yake ni kulinda viwanda, pia kuwalinda walaji.

Hapo alikuwa anazuru mkoani Morogoro katika uzinduzi wa upanuzi wa mashamba ya sukari na umwagiliaji, ili kuwa na kilimo cha uzalishaji wa kisasa.

"Tunalenga kufikisha sukari tunayozalisha Jamhuri ya Watu wa Congo (DRC) na nchi nyingine kwa kuzidi kuboresha miundombino ya usafiri na uzalishaji ili kupanua wigo wa masoko ndani na nje ya nchi kwa kuongeza tija," akasema Rais Dk. Samia.

Kiwanda hicho cha sukari kimefunga mitambo ya kisasa 47 inayofanya kazi kati ya 112 inayopaswa kujengwa, itakayoongeza uchakataji wa miwa kutoka tani 100 hadi 180 kwa saa.

Hapo kukafafanuliwa matarajio yake kwamba ni kufikia mwaka 2027 itachakata tani 230 za miwa kwa saa, ikiendana na kutolewa ajira zinazofika 10,000.

**MIPANGO VIWANDA ILIVYO**

Hatua za kuibua na kendeleza viwanda nchini, inatajwa kuwamo katika muhtasari wa Wizara ya Viwanda na Biashara, inatekeleza majukumu yake ya kimuundo kwa kuzingatia maelekezo ya viongozi wakuu wa serikali.

Kurejea miongozo ya wizara husika na viwanda, ni maelekezo yanayotajwa kuwamo katika mipango ya kitaifa na kimataifa, kama ilivyoainishwa kwenye Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs 2030), vilevile Ajenda ya Afrika 2063.

Maeneo mengine nchini yanatajwa kuwa ni: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Uchaguzi Mkuu ya Mwaka 2020; na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26.

Pia, katika kuchochea kasi ya ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini, wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaendelea kufanya mapitio ya Sera, Mikakati na Sheria za kisekta.

Hapo dhamira ni kuziwezesha kuendana na mahitaji ya sasa. Anazitaja sera hizo ni pamoja na sera za taifa za: Uhamasishaji Uwekezaji (1996); Mae

deleo Endelevu ya Viwanda (SIDP, 1996 - 2020); Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo (2003); Masoko ya Mazao ya Kilimo (2003); na Sera ya Taifa ya Biashara (2003).

Msukumo huo unaoibua viwanda nchini, inatajwa ni sehemu ya kazi za Wizara ya Viwanda na Biashara, ikienda sambamba na sheria, pia mikakati ya kisekta, ikiwamo inayoendeleza Sekta ya Ngozi na Bidhaa za Ngozi; Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Pamba, Nguo hadi Mavazi (C2C); Mkakati wa Kuendeleza Zao la Alizeti; Sheria ya Kujilinda dhidi ya Athari za Kibiashara; sheria za uwekezaji, pia ushindani ya mwaka 2003.

Viwanda, ndio suala linalotamba hivi sasa katika majukwaa ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ndani na nje ya Tanzania.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Mapaparazi tuombeane Heri ya Mwaka mpya, lakini...!




JAMANI wasomaji na mashabiki wa safu hii, nakutakieni heri ya mwaka mpya wa 2025. Ilikuwa ni safari ndefu ya milima na mabonde yenye mbu na kila aina ya bughudha za kisiasa, kijamii na kiuchumi.

Tuwaombee waliotangulia mbele za haki, tuwaombee walio na maumivu ili Mungu awape afueni warejee kulijenga Taifa lao, tuwaombee wanaotaka kutuongoza, wajipange vema ili mwaka huu tupate viongozi wazuri zaidi kuliko waliopo.

Nasema hivyo, kwani ni shauku ya kila mmoja wetu kupata viongozi stahiki wanaoweza kutuvusha kutoka lindi la umasikini lililotulalia hivi sasa na kukosa kufurukuta, kutokana na baadhi ya viongozi wetu kutumia migongo yetu kujinufaisha.

Nikirejea kwa wenzangu mapaparazi, ni mwaka wa kujisahihisha, kujirekebisha na kuachana na uchawa uliotamalaki miongoni mwetu, ukatupofusha na kushindwa kutazama tulikokanyaga na twendako.

Tumeshuhudia vyombo vya habari, baadhi vikishindwa kusimamia maadili na kujikuta vimevishwa na kukubali vilemba vya ukoka na kudhani vinakwenda vyema kumbe segemnege.

Hivi sasa si siri, tuna utitiri wa vyombo hususan magazeti yasiyo na kichwa wala miguu, yanayoandika chochote kinachojitokeza mbele ya waandishi au waandikaji wao, ili mradi kinatekenya wachache, huku yakishindwa kutambua umasikini uliotamalaki kwenye jamii.

Tumemkaribisha hivi karibuni mwanahabari mwenzetu na mwanasheria nguli, Profesa Palamagamba Kabudi kwa mikono miwili, tukiamini atatrudisha mstarini tulikokwishakengeuka na kukaa pembeni kipindi kirefu sasa.

Tukimpa ushirikiano wa dhati, Inshallah, atatuvusha na kurejea



NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com

tulikokuwa enzi hizo, tukiitwa waandishi wa habari au wanahabari, 'aka' Mhimili wa Nne wa Dola (kama ni kweli), na kuisaidia nchi kuona iliko na iendako.

Ni jambo la kushangaza na kusikitisha, kuwa hivi sasa tasnia ya habari imevamiwa, imeingiliwa kinyume cha kawaida na watu wasio na taaluma, ili mradi ni maarufu kwa futuhi na mambo mengine ya kichawachawa.

Hali ni mbaya zaidi katika vyombo vya kielektroniki, waliko watu wanaosingiziwa kuwa watangazaji, wanaosema chochote bila kujali msikilizaji anataka nini, ili mradi sema yao inawapa umaarufu mitaani, huku wakijiita majina bandia.

Ni wapi ulisikia taarifa ya habari inasomwa na mtu aliyejipachika jina bandia na watu wakamsikiliza kwa sababu tu eti ni msanii wa futuhi na vichekesho?

Tanzania hivi sasa inawezekana, ambako wasanii hukana majina yao ya kuzaliwa na kujipachika ya bandia.

Kama nilivyonena hapo juu, tuna magazeti lukuki yanayoandikwa na watu wachache, mtu mmoja anaandikia magazeti hata 10, stori ile ile na sentensi ile ile katika magazeti yote na hakuna anayejali, ili mradi yanatoka, ingawa mengi ya mitandaoni.

Hivi sasa kuna magazeti yanatoka ukurasa mmoja tu wa mbele, kama bango, lakini yanaungwa mkono na kushangiliwa na wenye mamlaka na kuonekana nayo miongoni mwa yanayoheshimika na kutajwa, ikiwezekana hata ruzuku yapewe. Ni ya kimkakati hayo!

Kuna vituo vya redio, visivyo na wajuzi na wataalamu wa habari, lakini vipo vinarusha matangazo kwa kutegemea vyombo vingine makini.

Mathalan, kituo kinakuwa na 'Kipindi cha Magazeti', watangazaji wake ambao wengi ni watu wa futuhi, wanachukua magazeti na kusoma 'lidi storis' za wenzao 'font fedi' na kugeuza zao.

Ni uvivu na umbumbumbu wa taaluma, ukiwazuia kujitafutia stori zao wakazisoma na kuzijadili!

Wakiruhusiwa kusoma vichwa vya habari, wao wanasoma habari yote na hata msikilizaji aliyekuwa na shauku ya kununua gazeti hatafanya hivyo tena na badala yake 'buku' lake, atalihamishia kununua mafuta ya taa kwa kuwa umeme nao hauaminiki bado.

Hiyo ni sawa na wafanyabiashara jirani; mmoja anauza vitumbua, mwingine viazi vya kuchemsha, huyu wa viazi ataachana na viazi vyake na kuamua kujadili vitumbua vya mwenzake huku akilalamikia sukari na mchanga na hatimaye kumkatisha tamaa mteja asinunue, hivyo hasara kwa mchoma vitumbua. Ikumbukwe tu, akiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk Harrison Mwakyembe, alipiga marufuku usomaji wa aina hiyo, ulioathiri vibaya mauzo ya magazeti na kusababisha malalamiko ya wamiliki.

Ina maana kila zama na kitabu chake, kwamba Mwakyembe alipoondoka akaondoka na agizo lake? Hapana! Tujirekebishe wahusika.

Tusimlazimishe Profesa Kabudi ashike mjeledi atushikishe adabu.Chakabhugane!

UCHUMI

## MWAKA INTANETI ZILIANZA...

# Matano kimaendeleo yaliyotabiriwa na watafiti 1995, yangeibukia mwaka huu

**Na Mwandishi Wetu**

MNAMO mwaka 1995, kulifanyika utabiri wa kiyaansi, namna ulimwengu utakavyokuwa miaka 30 baadaye, yaani 2025, leo ikiwa siku ya tatu.

Ilitangazwa kupitia kipindi cha radio na televisheni kimataifa, mwanazuoni Prof. Stephen Hawking, aliyetabiri kwamba: "Kufikia 2025, tunaweza kutarajia mabadiliko makubwa."

Akaelezea uvumbuzi tarajiwa, kwamba utatikisa ulimwengu kuanzia kwenye vifaa vya matibabu ya upasuaji hadi sekta ya anga.

Leo imetimu miongo hiyo mitatu, ikiwa na swali "utabiri huo umefanikiwa kuuangazia ulimwengu leo?



Prof. Stephen Hawking, ni sehemu ya utabiri wa mwaka 1995, kuhusu yanayojiri mwaka huu ulioanza juzi.**PICHA:MTANDAO.**

**MAFANIKIO YA INTANETI**

Mnamo mwaka 1995, intaneti zilianza kutumika duniani na maendeleo yake yakatabiriwa kisomi, yangeleta matatizo katika siku ambazo leo imetimu.

Ikatabiriwa "matajiri wakubwa" na benki zitachukua udhibiti wa intaneti kufikia 2000, na kuanzisha intaneti itakayokuwa na kasi zaidi na kudhibiti usambazaji wake.'

Hilo, kwa upande mmoja likatarajiwa lingesababisha udukuzi, virusi na hata ghasia.

Hadi sasa intaneti bado inatumiwa na watu wengi na haijaonekana ghasia, lakini hakuna vitendo vya wadukuzi vimesababisha kadhia kwa watu wengi watumiaji.

Kimoja ambacho kipindi hicho hakikutabiriwa ni kuhusika kwa wadukuzi wa taifa kama Korea Kaskazini.

**MADINI KUCHIMBWA ANGANI**

Kipindi hicho kukatabiriwa uchimbaji madini angani, ukibashiriwa kuwa sekta yenye faida kubwa, huku kampuni zikichimba kwenye miamba (asteroids) iliyo karibu na dunia, kwa ajili ya madini ya thamani.

Utabiri ukaeleza taka za angani zingehatarisha usalama wa wanaanga.

Kufikia mwezi huo, hakuna sekta ya uchimbaji madini nje ya sayari yetu, lakini hilo linaweza kubadilika.

Mtaalamu wa masuala yajayo, Tom Cheesewright, ana matumaini kuhusu uchimbaji madini nje ya sayari yetu.

"Utajiri uliokuwa ni mkubwa na teknolojia iko ndani ya uwezo wetu," anasema.

**ROBOTI KUFANYIWA UPASUAJI**

Pia, kukafafanuliwa wagonjwa wangefanyiwa upasuaji na roboti ambazo zinaongozwa na daktari wa upasuaji akiwa eneo lingine la mbali.

Ikatabiriwa kufikia mwaka 2004, sheria ingepitishwa kwa hospitali zote za Uingereza kuchapisha jedwali la viwango vya mafanikio ya upasuaji uliofanywa na madaktari wake.

Madaktari wakuu wa upasuaji wakatajwa wangekuwa maarufu sana na kulipwa vizuri, kusingekuwa na haja kwao kusafiri kufuata wagonjwa.

Pia, madaktari wa upasuaji wangefanya kazi kwa kutumia 'glovu' maalum na roboti zingeweza kuiga kikamilifu mienendo ya daktari wa upasuaji.

Hadi sasa - hilo halijawezekana kama hivyo, lakini roboti zinasaidia upasuaji.

**HUDUMA BENKI**

Swali linakuja, unajisikiaje kuhusu kutoa pesa kwa kutumia chipu iliyopandikizwa kwenye mkono wako?

Mahali pengine katika kipindi hicho, kulitolewa maono ya huduma zinazotarajiwa za kibenki.

Ilionesha mwanamke akienda benki, akilalamika hakuna wahudumu binadamu na kisha kutoa "kiasi cha Euro 100." Benki inampa pesa hizo baada ya kuskani chipu mkononi mwake.

Uhalisia sasa, huduma ya benki imekuwa ya kidijitali zaidi, ingawa kulipa kupitia 'chipu' ndani ya mwili wa binadamu ni jambo linalowezekana, teknolojia nyingine - hasa alama za vidole na uso - zinatumika zaidi.

**KUMBUKUMBU ZA WATANGAZAJI**

Nyota wa Dunia wa Sekta ya Kilimo cha Bustani, Monty Don, alikuwa mmoja wa watangazaji kwenye kipindi hicho miaka 30 iliyopita.

Sehemu yake ilitabiri urejeo mkubwa wa misitu ya Uingereza kutokana na uzalishaji wa vifaa vya kilimo na kusababisha kurudi kwa wanyama ikiwa ni pamoja na dubu wa kahawia.

Akitafakari kuhusu hilo sasa, akasema kwamba sehemu yake ya kipindi hicho ilikuwa haina uhalisia.

Akiangalia miaka 30 sasa, amefurahishwa na kizazi cha cha vijana "kinachoguswa zaidi na mabadiliko ya tabianchi" na anaamini watu watakuwa wakilima chakula chao zaidi ifikapo 2055.

Vivienne Parry alikuwa mtangazaji mwingine kwenye kipindi cha utabiri, na alikuwa na kipengele kilichozungumzia dawa.

Vivienne amejihusisha na taaluma hiyo tangu 2013 na anaangazia baadhi ya utabiri kutoka katika kipindi hicho cha 1995 kuhusu mpangilio wa vinasaba umetimia, anapofanyia utafiti ili kusaidia kutambua na kutibu hali za vinasaba.

**DUNIA ITAKUWAJE?**

Mtabiri Tracey Follows anaamini programu ya 1995 ilipatia tabiri nyingi kubwa sawa, lakini ikakosea mada mbili kuu za miaka 30 iliyopita - kuenea kwa makampuni ya teknolojia na mitandao ya kijamii.

Kufikia 2055, anafikiri watu wengi "watakuwa wameweza kuunganishwa kimawazo" - mawazo ya wanadamu na teknolojia kupitia 'seva', ambayo itasaidia katika kubadilishana mawazo.

"Kushirikishana kiakili kutakuwa kwa uhalisi, ambao utaweza kubadilishana mawazo na mtu mwingine kwa kuyafikiria tu."

Mtangazaji anafikiri matarajio mawili ya kusisimua zaidi kwa miaka 30 ijayo, yatakuwa maendeleo ya sayansi ya vifaa na matumizi ya 'tishu' bandia, viungo, au sehemu za kiungo kuchukua nafasi ya sehemu za mwili zilizoharibika au kutokokuwapo.

Kwa hivyo, Je, unadhani ulimwengu utakuwaje katika miaka 30 ijayo?

• *Kwa mujibu wa BBC*

# SERIKALI KATIKA MAPINDUZI MAENDELEO, KUPITIA UBUNIFU WA TEKNOLOJIA ZA VIJANA

Inatoka Uk 11

wa Elimu, Sayansi na Teknolijia, anasema serikali itaanza kuzitambua tafiti zinazofanyika kila mwaka, ikiwamo kuwatambua watafiti na kuwaongezea chachu ya ushawishi.

Anasema, wameamua kufanya hivyo kuongeza hamasa katika ufanyaji tafiti, pia kujua umuhimu wa watafiti wanaoleta tija kulingana na utafiti wao.

Waziri huyo anataja mfano kumrejea wasomi wenzake, akiwataja kwa jina moja, watafiti maprofesa; Manji na Misinzo, wakiendelea kutambua watafiti wengine.

Hilo Waziri anasema, wameshafanya tafiti zilizosaidia kutatua changamoto kwa taifa, kwamba kila mwaka inasaidia kazi za nchi kujulikana ndani na nje ya nchi.

**DK. DOTO BITEKO**

Naibu Waziri Mkuu, ambaye ana dhamana ya Waziri wa Nishati, Doto Biteko, anasema watafiti na wabunifu wa ndani nchini, wanapaswa kutambuliwa na kupewa fursa ya kuchangia maendeleo ya taifa.

Hapo anasisitiza kuwa, ili Tanzania ifikie malengo yake ya kiuchumi na kisayansi, ni muhimu kutambua na kuwekeza katika ubunifu wa wanasayansi wa ndani, ambao ndio msingi wa maendeleo endelevu.

Dk. Biteko anasema serikali imejizatiti kuwapa wanasayansi na wabunifu wa ndani nafasi ya kuleta mabadiliko chanya katika sekta mbalimbali, zikiwamo kilimo, afya, nishati na usafiri.

Anafafanua kuwa, kupitia utafiti na ubunifu, watafiti wataweza kutatua changamoto za kijamii na kiuchumi zinazokabili taifa, hivyo inachochea maendeleo.

Dk. Biteko anasema, watafiti na wabunifu wa ndani wanahitaji kutambuliwa kama sehemu muhimu ya mageuzi ya kijamii na kiuchumi na serikali imejizatiti kutoa mazingira bora ya kufanya tafiti na ubunifu kwa kuweka sera rafiki kwa wanasayansi, kuongeza rasilimali za kifedha na kuhakikisha kuwa miundombinu ya utafiti inaboreshwa ili kuwezesha tafiti za kisayansi.

"Watafiti wa Tanzania wanapaswa kuwa na fursa ya kutumia uwezo wao kubuni suluhu za kisayansi ambazo zitakuwa na manufaa kwa taifa, hivyo tutahakikisha kuwa tunawawezesha kufanya tafiti ambazo zitasaidia kuimarisha kilimo, kuboresha huduma za afya, na kutoa ufumbuzi wa nishati endelevu," anasema Dkt. Biteko.

Anafafanua kuwa, COSTECH imeanzisha mifumo ya kutoa ufadhili wa tafiti na kutoa msaada kwa wabunifu wa teknolojia, ili kuongeza ubora wa tafiti zinazofanyika nchini ili kuwawezesha wanasayansi na wabunifu kuchangia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya nchi.

Pia, imetenga fedha za kuanzisha na kuendeleza taasisi za utafiti, ikitoa vifaa vya kisasa vya kufanya tafiti.

Hiyo ni pamoja na kuhamasisha ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, ili kubuni na kuendeleza teknolojia za kisasa zinazoweza kutatua matatizo ya jamii. Katika kuimarisha uwezo wa wanafunzi na vijana, Dk. Biteko anaeleza ni muhimu kwa Tanzania kuongeza uwekezaji katika elimu ya sayansi na teknolojia, hasa kwa vijana na wanawake, ili kuwapa ujuzi na mitaji ya kuwa wabunifu wa baadaye.



# Nyuki kuwatimua tembo kwenye makazi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KIJIJI cha Nyuki Co.Limited Halmashauri ya Manispaa ya Singida kimetangaza mkakati wake kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii kudhibiti tembo kuvamia makazi ya wananchi na kuharibu mali kwa kutumia nyuki.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kijiji hicho, Phillemon Kiemi akizungumza juzi na waandishi wa habari, alisema hatua hiyo inatokana na usumbufu wanaopata wakazi wa Mkoa wa Singida kwa kuvamiwa na tembo kwenye makazi yao mara kwa mara.

Kemi, alisema kijiji chao kinachojishughulisha na ufugaji nyuki, mwaka huu kimekuja na mbinu za kisasa kuwadhibiti wanyama hao.

Alisema mapito ya tembo kwenye wilaya za mkoa huo zinazopata usumbufu wa wanyama hao, yataainishwa kisha kuweka mitego ya mizinga ya nyuki ambayo itatumika kuwafukuza kwenye makazi.

"Kutumia wataalam wabobezi wa kijiji cha nyuki, tutatumia mbinu za kukabiliana na tembo hao kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na utalii," alisema.

Kiemi alitaja mikakati mingine ambayo wamepanga kufanya kwa mwaka huu kuwa ni kufungua ranchi ya ufugaji wa malkia wa nyuki.

Alisema lengo ni kusaidia kupunguza changamoto ya upungufu wa nyuki ambao kwa sasa unalalamikiwa na wafugaji wa nyuki nchini.

**Kazi nyingine zitakazofanyika ni kufungua viwanda vya kuzalisha mvinyo wa asali, kujenga hoteli na viwanja vya mpira ili timu kubwa...**

Alisema mwaka huu wamepanga kutoa mafunzo kwa watu 10,000 kutoka vijiji vyote vya Mkoa wa Singida namna ya ufugaji nyuki na kuwapa mzinga kila mmoja ili waanzishe mradi huo.

Kazi nyingine zitakazofanyika ni kufungua viwanda vya kuzalisha mvinyo wa asali, kujenga hoteli na viwanja vya mpira ili timu kubwa nchini zitakapowasili Singida zifikie kijini kwao kufanya utalii na kupata huduma ya malazi.

Kumekuwa na mfululizo wa matukio ya tembo kuvamia makazi ya watu na kubomoa nyumba katika Mkoa wa Singida.

Novemba 10, mwaka jana tembo zaidi ya 56 walivamia Kijiji cha Mkiwa wilayani Ikungi, kuvunja nyumba nane na kula vyakula.

Kufuatia tukio hilo, wakazi wa Kijiji hicho walifunga barabara kuu ya Dodoma -Singida na kumlazimu Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Pindi Chana kufika na kuagiza askari wa TAWA kuweka kambi kuwadhibiti wanyama hao.

Kwa Mkoa wa Singida wilaya nyingine zinazokabiliwa na tatizo la tembo hao ni Manyoni, Singida na Halmashauri ya Itigi.



Kaimu Ofisa Maendeleo Jiji la Dodoma, Hidaya Mizenga akitoa mada kwa viongozi wa majukwaa ya wanawake kwenye mafunzo kwa ajili ya kuwapatia fursa za kiuchumi na mikopo ya asilimia 10 iliyofanyika Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wajasiriamali 6,500 wapigwa msasa

**Na Thobias Mwanakatwe,** ITIGI

WAJASIRIAMALI 6,500 wa kata 13 za Halmashauri ya Itigi, mkoani Singida wameanza kupatiwa mafunzo ya kujikwamua na umaskini na kukidhi vigezo vya kupata mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na serikali kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Itigi, Saimon Sirilo, juzi aliwaambia waandishi wa habari kuwa anaendesha mafunzo hayo kwa kujitolea.

Sirilo, alisema alianza kutoa mafunzo hayo tangu Januari mwaka jana kwa wajasiriamali hao ili wapate mbinu za kuanzisha biashara ndogondogo na kujikwamua kiuchumi na kuunda vikundi na kupata mikopo hiyo ya serikali inayotolewa kupitia halmashauri.

Alisema, mafunzo anayoyatoa ni pamoja na kutengeneza sabuni ya maji, batiki, karanga za mayai, elimu ya fedha, kupanga bajeti, huduma kwa wateja na kutafuta masoko.

Sirilo, alisema hadi Desemba mwaka jana ametoa mafunzo hayo kwa wajasiriamali wa kata za Majengo, Itigi Mjini, Tambukareli, Ipande, Sanjaranda, Aghondi, Mgandu, Mitundu, Mwamagembe na Kitaraka.

Alisema kata zilizobaki za Kalangali, Rungwa na Idodyandole, anatarajia kuanza kutoa mafunzo hayo mwezi huu.

"Mafunzo hayo nayatoa bure katika maeneo yote kama sehemu ya utumishi wangu kuwahudumia wananchi nikiamini jamii ikikombolewa kimaarifa na kiuchumi basi taifa limepona na tutakuwa na maendeleo makubwa katika taifa letu," alisema.

Sirilo aliwashukuru viongozi wa kata hususani madiwani ambao katika kila kata anayokwenda kutoa mafunzo amekuwa akipata ushirikiano mzuri na kufanyika kwa ufanisi mkubwa.

Mwishoni mwa mwaka jana, Halmashauri hiyo ilitoa wito kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kuomba mikopo zaidi ya Sh.milioni 442.755 ambazo zimetengwa kwa ajili ya vikundi hivyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Ayoub Nkambi, alisema fedha hizo zilianza kutengwa katika robo ya kwanza ya Julai-Septemba ya mwaka huu wa fedha 2024/2025.

" Vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kuleta maombi katika ofisi za serikali za vijiji zilizopo katika maeneo yao," alisema.

Nkambi alitaja sifa za vikundi vinavyotakiwa kuomba mikopo hiyo kuwa kinachotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na halmashauri, kinachojishughulisha na ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli hizo za ujasiriamali. Nyingine ni kwa kikundi cha wanawake na vijana chenye idadi ya wanakikundi kuanzia watano na kuendelea na watu wenye ulemavu kiwe wasiopungua wawili.

# Taasisi zaamriwa kuondoa mabango barabarani

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MENEJA wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) mkoani hapa, Edward Lemelo amewaamuru wananchi na taasisi zenye mabango yaliyowekwa barabarani bila kufuata utaratibu kuyaondoa haraka kabla sheria kuanza kuchukua mkondo wake.

Lemelo, alitoa amri hiyo jana wakati akizungumza na Nipashe kuhusu utaratibu wa mabango hayo yaliyowekwa barabarani.

"TARURA tunawataka wale wote walioweka mabango ya biashara na mengine kuondoa haraka kwa sababu tutakuwa na zoezi la kuondoa mabango hayo yaliyowekwa vibaya, " alisema

Alisema ni kosa kuweka bango kwenye makutano ya barabara bila kibali cha mamlaka husika kwa sababu kunaweza kusababisha ajali kwa watumiaji wa miundombinu hiyo.

Lemelo, alisema TARURA haizuii mabango, isipokuwa wanataka yawekwe mbele ya maeneo yao ya biashara au sehemu ambayo haizuii watumiaji wa barabara.

# Watakiwa kudhibiti utoro wa wanafunzi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WENYEVITI wa vitongoji wa Kata ya Hogoro ya Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa mkoani hapa wametakiwa kushirikiana na wazazi na walezi kudhibiti utoro wa wanafunzi shuleni na kuwajengea nidhamu.

Rai hiyo imetolewa na Diwani wa Kata ya Hogoro, Mtwanga Sadala wakati wa hafla ya kukabidhiwa miundombinu na wahandisi wasio na mipaka kutoka Marekani iliyofanyika katika Shule ya Sekondari Banyibanyi iliyopo wilayani humo hivi karibuni.

Sadala, alisema wenyeviti hao wanapaswa kuelekeza jitihada kuwasaidia wazazi na walezi kuhimiza mahudhurio ya wanafunzi shuleni ili kudhibiti utoro shuleni na mmonyoko wa maadili.

Alisema wakiwaona wanafunzi wanazagaa mitaani wakati wa masomo wanapaswa kuwauliza changamoto zinazowakabili na kuwahimiza wahudhurie masomo ya darasani na kuwa viongozi bora wa baadaye.

Aliwashukuru wahandisi hao kwa kukabidhi baiskeli kwa wanafunzi 35 wa sekondari hiyo na kuwaondolea adha ya kutembea umbali mrefu kutoka nyumbani kwao hadi shuleni na kurudi..

Akizungumza baada ya kukabidhiwa baiskeli hizo, Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Magreth Temu, aliwashukuru wahandisi hao kwa kupunguza changamoto ya wanafunzi hao kutembea umbali mrefu na kukosa baadhi ya vipindi kwa kuchelewa kufika shuleni.

Magreth, alisema wahandisi hao, pia wamejenga nyumba ya mwalimu, matundu 12 ya vyoo, miundombinu ya kuvuna maji ya mvua na chumba cha kompyuta kwa ajili ya masomo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika Shule ya Msingi Mkutani.

Diwani wa Hogoro , Mtwanga Sadala aliwataka wenyeviti wa vitongoji kushirikiana na wazazi kushughulikia utoro wa wanafunzi shuleni na kuwasihi wanafunzi kuwa na nidhamu kwa walimu na jamii.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mkutani, Samwel Chidabile, aliwashukuru wahandisi kwa kuwa marafiki bora tangu mwaka 2017 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya shule hiyo.

Alisema mpaka sasa, wamepokea baiskeli 121 ambazo zinasimamiwa na kamati ya shule kuhakikisha zinakuwa salama na kutumiwa kwa wanafunzi wa sekondari hiyo.



# Watendaji waagizwa kutunza vifaa uandikishaji wapigakura

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), imewaagiza watendaji wa uboreshaji Daftari la Kudumu la Wapigakura kutunza vifaa vita kavyotumika ili vipelekwe maeneo mengine nchini na kuipunguzia serikali gharama ya kununua vingine.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Mjumbe wa INEC, Jaji Asina Omari wakati akizindua mafunzo ya siku mbili kwa watendaji hao ngazi ya Mkoa wa Njombe yaliyofanyika mjini hapa.

Jaji Asina, alisema kutokuwa makini katika utunzaji wa vifaa hivyo, kutapelekea athari kubwa kukamilisha zoezi hilo muhimu kwa muda uliopangwa na tume hiyo.

"Mnapaswa kuzingatia maelekezo yote yatakayotolewa na tume ili muweze kuyafanyia kazi wakati zoezi litakapokuwa limeanza na matokeo yanategemea ushirikiano mkubwa kati ya watendaji wote wa uboreshaji, serikali, vyama vya siasa na wadau wengine wa uchaguzi," alisema Jaji Asina.

Alisema mafunzo hayo yatahusisha ujazaji fomu na kutumia mfumo wa kuandikisha wapigakura ili kupata uelewa wa kutumia kwa ufasaha mfumo huo pamoja na vifaa vingine.

**"Na kikundi kikishindwa hili niliseme wazi kikishindwa kurejesha zipo sheria ambazo zimetungwa kwa ajili ya kukiwajibisha hicho kikundi," alisema Mwansasu.**

"Mafunzo haya yanalenga kuwajengea umahiri wa kuwafundisha maofisa uandikishaji wasaidizi ngazi ya kata, kisha nao watatoa mafunzo hayo kwa waendeshaji wa vifaa vya bayometriki na waandishi wasaidizi ambao ndiyo watahusika na uandikishaji wapigakura vituoni," alisema.

Alisema maofisa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) watapatiwa mafunzo maalumu ya kukabiliana na changamoto za kiufundi wakati wa uandikishaji wapigakura vituoni.

Alisema katika zoezi la uboreshaji daftari hilo, mawakala wa vyama vya siasa wataruhusiwa kuwepo katika vituo vya kuandikisha wapigakura kuleta uwazi.

"Pia mawakala hao watasaidia kutambua waombaji wa eneo husika hivyo kupunguza kutokea kwa vurugu zisizokuwa za lazima," alisema.

Alisema mawakala au viongozi wa vyama vya siasa hawaruhusiwi kuingilia mchakato wa uboreshaji wa daftari hilo.

Mafunzo hayo ni maandalizi ya uboreshaji wa daftari hilo utakaofanyika kwa siku saba kuanzia Januari 12 hadi 18, mwaka huu mkoani hapa.

Mafunzo hayo yanafanyika wakati taifa linajiandaa kwa uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani utakaofanyika Oktoba mwaka huu.



Maofisa wa uandikishaji na uboreshaji wasaidizi wa daftari la kudumu la wapigakura mkoani Njombe wakiapa kiapo cha kutunza siri pamoja na kiapo cha kujitoa kwenye vyama vya siasa. **PICHA: ELIZABETH JOHN**

# Waishukuru serikali kwa gari la wagonjwa

**Na Mwandishi Wetu,** LUDEWA

WAKAZI wa Wilaya ya Ludewa mkoani Njombe wameishukuru serikali kwa kuendelea kuboresha huduma bora za matibabu na kunusuru maisha yao.

Walitoa shukrani hizo juzi baada ya kukabidhiwa gari la kubeba wagonjwa na pikipiki mbili kwa ajili ya kubeba wagonjwa.

Walisema msaada huo utawaondolea adha wajawazito na wagonjwa kukosa usafiri wa haraka kuwahishwa hospitali ili kuokoa maisha yao.

Mary Mlelwa alisema, kitendo cha serikali kuwapatia gari hilo kitasaidia wagonjwa kuwahi hospitali, kupata matibabu haraka na kuokoa maisha yao.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Ludewa, Dk. Isack Chussi, alisema wilaya hiyo ni moja ya wilaya yenye vituo vingi vya afya ambavyo uhitaji wa usafiri wa vyombo vya moto ni muhimu zaidi kutokana na jiografia ilivyo.

"Hospitali, vituo vya afya na zahanati kwa ujumla vipo 81, msaada huu umerahisisha mgonjwa anapopata changamoto au dharura usafiri huo unamfikisha haraka," alisema Dk. Chussi.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Castory Kibasa, alisema gari na pikipiki hizo vimetolewa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ili kupunguza adha ya kusafirisha wagonjwa kutoka eneo moja la huduma hadi jingine.

Mbunge wa Ludewa, Joseph Kamonga pamoja na kuishukuru serikali kwa msaada huo, ameahidi kuendelea kushirikiana na wananchi kuleta maendeleo ya wilaya hiyo.

# CCM chaonya makada wake kampeni za mapema

**Na Mwandishi Wetu,**
NJOMBE

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe kimewaonya kuwa kitawachukulia hatua makada wake wanaonyemelea ubunge na udiwani katika majimbo kabla ya wakati.

Vilevile kimewaagiza viongozi wa chama hicho mkoani hapa kuchukua hatua kali hasa dhidi watu wanaoingilia shughuli za wabunge na madiwani kabla ya muda wao kwisha.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Katibu wa Siasa, Mafunzo na Uenezi CCM wa mkoa huo, Josaya Luoga wakati akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kikao cha halmashauri kuu ya chama hicho.

Luoga, alisema wabunge na madiwani waliopo wanapaswa kufanya kazi zao mpaka nafasi zao zimekoma.

"Hivyo halmashauri kuu imewaelekeza kamati za maadili kwenye majimbo na wilaya zote kuhakikisha wanapata taarifa za kutosha juu ya wanachama na viongozi wanaofanya kazi ya kuwa makuwadi wa wagombea wanaodhani wangetamani wawe viongozi 2025 kuelekea 2030," alisema Luoga.

Alisema kanuni za uongozi na maadili za CCM za mwaka 2021 zinaeleza mambo yasiyotakiwa kufanywa na mwanachama wa chama hicho anayetamani kugombea nafasi kwenye ngazi fulani.

"Mambo ambayo baadhi yanakatazwa ni kutoa michango, misaada, zawadi pasipokuwa na taarifa rasmi na vikao rasmi na kuidhinishwa na ngazi husika kwa maana kama ni wilaya iidhinishe michango hiyo, kama mdau anaitoa apite kwa katibu na uongozi ufahamu hana madhara kwenye utekelezaji wa ilani ya mwaka 2020/2025," alisema Luoga.

Aliitaja kanuni ya pili ni kwamba wapo viongozi wanakusanya michango kwa watu wanaodhani wanawatengeneza kwa nafasi hasa ubunge na udiwani.



# Wafamasia wahadharishwa janga vimelea sugu

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui amewahadharisha wafamasia nchini kuacha kutoa dawa holela ili kukabiliana na janga la vimelea sugu linalowanyemelea wananchi kwa kukosa tiba.

Mazrui, alitoa tahadhari hiyo jana wakati akizindua kampeni ya utoaji elimu kwa jamii kuhusu usugu wa vimelea dhidi ya dawa, iliyofanyika Chuo cha Afya Imperial College, Kisauni Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja.

Alisema wafamasia wana jukumu la kutoa elimu ya matumizi sahihi ya dawa kwa wagonjwa kufuata ushauri wa daktari ili kuiepusha jamii na madhara hayo. Mazrui, alisema maradhi yanayosababishwa na usugu wa vimelea dhidi ya dawa ikiwemo figo kushindwa kufanya kazi yataendelea kuwepo kama dawa zitaendelea kutolewa kwa wagonjwa kiholela.

Alisema Serikali ya Zanzibar inatambua na kuthamini juhudi za wadau wanaowekeza katika sekta ya afya kusaidia kuimarisha afya za wananchi.

"Nivipongeze vyuo vya afya na wadau wengine kwa kusaidia Serikali kutoa elimu kwa jamii kuhusu usugu wa vimelea dhidi ya dawa" alisema Mazrui.

**"Dawa zinaposhindwa kufanya kazi maradhi ya maambukizi yataibuka kila siku na yatahitaji kutibiwa kwa dawa zile zile ambazo zimekua hazitibu tena ugonjwa husika**

Daktari Muhudini Omar kutoka Wizara ya Afya Idara ya Kinga, alisema usugu wa vimelea dhidi ya dawa ni ugonjwa unaoua kimyakimya.

Kwa mujibu wa Omar, inakisiwa kuwa kati ya vifo milioni 50 vya watu vinatarajiwa kutokea hadi kufika mwaka 2050 kutokana na ugonjwa huo.

"Dawa zinaposhindwa kufanya kazi maradhi ya maambukizi yataibuka kila siku na yatahitaji kutibiwa kwa dawa zile zile ambazo zimekua hazitibu tena ugonjwa husika kutokana na kushindwa kutibu vimelea vilivyomo mwilini," alisema.

Mganga kutoka Chuo cha Afya cha Glorious Polytechnic, Mustafa Daud, alitaja miongoni mwa sababu zinazopelekea tatizo la usugu wa vimelea mwilini kuwa ni pamoja na utumiaji wa vijiua sumu kiholela, kukatisha dozi, kutumia dawa bila ushauri wa daktari na kutoa dawa bila kufuata miongozo sahihi iliyowekwa.

Daud, alisema vyuo vya afya, wafamasia na wadau wengine, wataendelea kushirikiana na Serikali kuhakikisha kunakuwa na miongozo madhubuti ya matumizi ya dawa na kuinusuru jamii na janga hilo.

"Tutaendelea kuelimisha jamii juu ya usugu wa vimelea dhidi ya dawa ili kudhibiti matumizi mabaya ya vijiua sumu na kulinda afya za watu," alisema.

Kampeni ya uelimishaji jamii juu ya usugu wa vimelea dhidi ya dawa imeandaliwa na Jumuiya ya Wafamasia Tanzania (TAPSA) kwa kushirikiana na vyuo vya afya vilivyopo Zanzibar.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mahmoud Thabit Kombo (kulia) akizungumza na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Dk Haroun Ali Suleiman katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi Mahakama ya Wilaya huko Kisakasaka Nje ya Mji wa Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Tuache siasa za chuki, uhasama - Waziri

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANANCHI visiwani hapa wametakiwa kuachana na siasa za chuki na uhasama na kuunga mkono juhudi za Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kuwaletea maendeleo kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mohamed Mussa wakati wa hafla ya kuweka jiwe la msingi ujenzi wa Shule ya Sekondari Kifundi Wilaya ya Micheweni mkoani Kaskazini Pemba.

Lela, alisema siasa hizo kwa Zanzibar zimepitwa na wakati na hazina faida kwa wananchi na wanachotakiwa ni kuendelea kuunga mkono juhudi za Dk. Mwinyi za kuendelea kuwaletea maendeleo.

Aliwataka wakazi hao wa Kaskazini Pemba kuunga mkono na kuthamini jitihada ambazo kiongozi huyo amekuwa akizifanya kuwaletea maendeleo tangu alipoingia madarakani.

Akizungumzia kuhusu bajeti ya Wizara ya Elimu, alisema imeongezeka na kufikia Bilioni 800 kwa lengo la kuhakikisha watoto wanasoma katika mazingira bora, shule zenye hadhi na kukidhi mahitaji ya kusomea na kufundishia ikiwa ni dhamira njema ya waasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar.

Awali akiweka jiwe la msingi la ujenzi huo, Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, alisema ujenzi wa miundombinu ya shule za ghorofa zinazoendelea kujengwa Kaskazini Pemba itasadia kuondoa msongamano wa wanafunzi darasani na kuongeza kiwango cha ufaulu.

Abdullah, alisema kuimarika kwa sekta ya elimu nchini kutawakomboa vijana na umasikini kwa kuzalisha wataalamu wazalendo wa fani.

Aliwataka walimu kuwa na mioyo ya uzalendo kufundisha na kuwalea vijana katika malezi yenye maadili.

Aliwaahidi walimu hao kuwa Serikali itaendelea kuangalia maslahi yao bajeti itakaporuhusu ili kulinda heshima na hadhi yao ikiwa ni fikra na falsafa za waasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha alisema azma ya Rais Dk. Mwinyi ya kukifungua Kisiwa cha Pemba kiuchumi inaanza kuzaa matunda kwa wawekezaji kutoka mataifa mbalimbali kuonesha nia ya kuwekeza kisiwani humo hasa Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Aliwasisitiza wananchi wa Konde na Wazanzibari kuendelea kudumisha amani, upendo, mshikamano, kuyaenzi na kuyalinda Mapinduzi ambayo ndio chachu ya maendeleo visiwani hapa.

Katibu Mkuu Wizara hiyo, Khamis Abdulla Said, alisema ujenzi wa sekondari hiyo utakapokamilika itakuwa na uwezo wa kuchukua wananfunzi 810 kwa mkondo mmoja, ikiwa ni wastani wa 45 kila darasa.

Saidi, alisema sekondari hiyo inayojengwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kiuchumi ya Afrika (BADEA) hadi kukamilika itagharimu shilingi Bilioni 9.47.

Alisema ujenzi huo unajumuisha madarasa, ofisi za walimu, dakhalia mbili kwa wasichana na wavulana, mgahawa na vyoo zaidi ya 30

# Balozi aainisha changamoto mahakama Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BALOZI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mahmoud Thabit Kombo amesema mahakama za Zanzibar zinakabiliwa na changamoto ya miundombinu ya majengo na kusababisha usumbufu kwa watendaji wa idara hiyo.

Balozi Kombo aliyasema hayo jana wakati akiweka jiwe la msingi katika Mahakama ya Wilaya huko Kisakasaka visiwani hapa.

Alisema kutokana na changamoto hiyo kuikabili Zanzibar kwa miaka mingi, kulikuwa hakuna mazingira rafiki ya kufanyia kazi kwa watendaji.

Alisema hadi sasa bado baadhi ya mahakama zinaendelea kujibanza katika majengo ambayo hayana hadhi.

Balozi Kombo, alitoa mfano wa shughuli za Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini Unguja kuhamia jengo la Mahakama ya Watoto huko Mahonda.

Alisema Mahakama ya Wilaya ya Kaskazini A nayo baada ya jengo walilokuwa wakilitumia kuharibika imehamisha shughuli zake Mahakama ya Ardhi.

"Kwa ujumla mahakama zetu hazikuwa na majengo stahiki, nafasi za kutosha na mazingira yasiyo rafiki," alisema.

Alisema hali hiyo imepelekea Serikali kuchukuwa hatua za makusudi kuja na mradi wa ujenzi wa majengo ya mahakama za mikoa na wilaya Unguja na Pemba likiwemo jengo hilo.

Alisema ujenzi wa jengo hilo ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa majengo saba katika mwaka wa fedha uliopita wa 2023/2024.

Waziri wa Nchi ,Ofisi ya Rais, Katiba , Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Dk Haroun Ali Suleiman, alisema kujengwa kwa mahakama hizo kuna lenga kuongeza ufanisi wa kazi kwa watendaji wa idara hiyo na kwenda na wakati uliopo.

Mtendaji Mkuu wa Mahakama Zanzibar, Kai Bashir Mbarouk, alisema kuwa jengo hilo la kisasa linakidhi vigezo vyote, ikiwemo miundombinu kwa watu wenye ulemavu.

# Wakulima mpunga watakiwa kuzingatia mbegu za kisasa

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

BARAZA la Mchele Tanzania (RCT), limewashauri wakulima wa zao la mpunga kujikita katika matumizi ya mbegu za kisasa zinazoendana na matumizi sahihi ya mbolea na udongo uliopimwa ili kujua mahitaji na virutibisho vinavyohitajika.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Baraza hilo, Geofrey Rwiza, alisema hayo wakati wa kuhitimishwa kwa mradi wa kujenga uwezo kubadilishana uzoefu masuala ya uongezaji wa thamani katika zao la mpunga ulianza kutekelezwa mwaka 2020 na kufikia tamati Desemba 2024.

Alisema matumizi hayo yanachangia kupatikana kwa ubora wa zao hilo na kupata kiwango bora cha mchele wa daraja la kwanza na kuwanufaisha wakulima katika soko la ndani na nje ya nchi.

Aidha, alisema kwa sasa matumizi ya mbegu bora yasiyoendana na aina ya mbolea inayopaswa kutumika yamechangia zao la mpunga kushinmdwa kupatikana kwa wingi mchele wa daraja la kwanza nchini.

"Hivi sasa mbegu nyingi zinazoendelezwa zinaendana vizuri na matumizi ya mbolea ikiwamo ya Natrojeni hivyo wakulima lazima wangalie hilo pamoja na kuangalia soko," alisema Rwiza.

Alisema kwa sasa Baraza hilo linawahamasisha wakulima wa zao hilo kuzingatia matumizi ya mbegu za kisasa na kuambatana na matumizi sahihi ya mbolea na kuvuna kwa wakati.

"Teknolojia hizo zitasaidia kurudisha hali ya kupata viwango vya mchele utakaopangwa kimadaraja na hasa uwingi wa upatikanaji wa mchele wa daraja la kwanza nchini," alisema Rwiza.

Kuhusu mbegu za kienyeji ambazo hazitumii mbolea, alisema kuwa mchele wake ukipangwa kwenye madaraja unapatikana kuwa ni mzuri kwa sababu ya kutotumia hizo mbolea.

"Nashauri matumizi sahihi ya mbolea na udongo yawe umepimwa ili kujua unahitaji virutubisho gani na si kuweka mbolea tu, pia kuweka kwa wakati unaopaswa ili maji yanapoingia shambani kusiwe na kupishana lengo kuwe na kalenda ya uwekaji mbolea na uvunaji kwa wakati," alisisitiza Rwiza.

> **"Nashauri matumizi sahihi ya mbolea na udongo yawe umepimwa ili kujua unahitaji virutubisho gani na si kuweka mbolea tu, pia kuweka kwa wakati unaopaswa ili maji yanapoingia shambani kusiwe na kupishana lengo kuwe na kalenda ya uwekaji mbolea na uvunaji kwa wakati," alisisitiza Rwiza.**

Mmoja wa wakulima wa Kijiji cha Wami Dakawa, Wilaya ya Mvomero, mkoani Morogoro, Nyaguso Lemwai, alisema amenufaika na mafunzo ya kilimo endelevu cha mpunga chini ya mradi huo ambao ulilenga namna bora ya matumizi ya mbegu bora za mpunga.

Alisema pia namna ya kuendesha kilimo cha kitalu mkeka kwa maana ya kutumia mbegu chache katika eneo kubwa na matumizi sahihi ya mbolea na maji ikiwa na matumizi ya zana bora za kilimo hicho na kuwezesha kuongeza kiwango cha uzalishaji na kipato kukua.

# Watoto sita wazaliwa mkesha wa Mwaka Mpya

**Na Steven William, MUHEZA**

WATOTO sita wamezaliwa wilayani Muheza mkoani Tanga katika Hospitali Teule ya Wilaya ya Muheza usiku wa kuamkia Mwaka Mpya 2025.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Dk. Fani Mussa, alitoa taarifa hiyo juzi kueleza kuwa afya za watoto hao na mama zao zinaendelea vizuri.

Dk. Mussa alisema kuwa katika idadi ya watoto hao watatu ni wa kiume.

Alisema watano wamezaliwa katika Hospitali Teule ya Wilaya ya Muheza na mtoto mmoja amezaliwa katika Hospitali ya Wilaya ya Samia Suluhu.

Dk. Mussa alisema kinamama wote sita waliojifungua hali zao na watoto wao zinaendelea vizuri na wote wanafuraha kupata watoto wakati wa mkesha wa Mwaka Mpya wa 2025.

Katika hatua nyingine Dk. Mussa alimshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa vifaa katika hospitali na vituo vya afya wilayani Muheza hali iliyosaidia kupunguza vifo vya kinamama na watoto wakati wa kujifungua.

Muuguzi wa zamu katika wodi ya wazazi katika Hospitali Teule ya Wilaya ya Muheza, Neema Ngoda, alisema ni jambo la furaha kuona kinamama wanajifungua salama na hakuna vifo vya watoto.

Alisema serikali imefanya jitihada kubwa za kuimarisha na kuboresha sekta ya afya kwa kuleta vifaa vya kisasa na dawa katika hospitali na vituo vya afya wilayani Muheza.

Alisema ni jambo la kumshukuru Mungu kwa kuona vifo vya kinamama na watoto nchini vinapungua.

## KUPOTEA KWA VYETI



**AMBELE ANOSISYE MBUGULU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.1264-0044 kilichotolewa na BWAWANI SECONDARY SCHOOL mwaka 2011. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba S.0681-0528 kilichotolewa na IVUMWE HIGH SCHOOL mwaka 2014. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/617/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GEOFREY GWIDO MGOVANO**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI T 955 ASF KWA JINA LA MATESO .S. SANGA AINA YA TOYOTA S.WAGON ILIYOPOTEA. KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE. POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/25/2025.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**IBRAHIM AYOUB DHAHABU** anatangaza kupotelewa na vyeti. Kidato cha nne index namba **S1189/0224 BIAFRA SECONDARY SCHOOL** mwaka **2008.** Kidato cha nne index namba **P0222/0422 ZANAKI CENTRE** mwaka 2009. Kidato cha sita index namba **S0496/0763 JITEGEMEE SECONDARY SCHOOL** mwaka **2012.** Taarifa za polisi: **PHQ/DAR/TEM/291926/2024, PHQ/TAN/LUS/14362/2024, PHQ/TAN/LUS/14374/2024.**

**IN THE DISTRICT COURT OF ARUMERU**
**AT ARUMERU**
**CIVIL CASE NO. 19 OF 2024**
**JOHN NDELILIO PALLANGYO ..........PLAINTIFF**
**VERSUS**
**GABRIEL ISACK AKYOO............................DEFENDANT**

**NOTICE OF DATE OF HEARING/MENTION**

**Rule 13 subordinate courts (Civil Procedure, Summoned & Plaintiff rules, 1955 G.N.No. 292/87) Cap.2 Sup.34).**

**To: GABRIEL ISACK AKYOO**
**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention/hearing in the District Court of Arusha at Arumeru on the 16th day of January 2024 At 8:30 am o'clock in the forenoon. You may appear in person or by Advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and your are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.
**TAKE FURTHER NOTICE** That in default of your appearance on that day time before mention or hearing the Court may proceed in your absence.
GIVEN Under my hand and the seal of the court this 19th day of December 2024.

RESIDENT MAGISTRATES
ARUMERU

## KUPOTEA KWA KADI ZA BAJAJI

**JUSTIN JOSEPH KIHONGO**
anatangaza kupotelewa na kadi tatu za bajaji za mizigo zenye namba za usajili MC.191 DUX, MC.201 DUX na MC.800 DTK zenye majina ya DEA TRADERS COMPANY LIMITED. Yeyote atakayeziona atoe taarifa kitup cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya polisi: **PHQ/SHI/KAH/12957/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI




**LUCIA RAMADHAN SHEKIVULI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S4024.0049** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **USAMBARA GIRLS SECONDARY SCHOOL** mwaka 2017. Cheti kilipotelea Mkwawa Iringa. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/IRI/IRI/20807/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MBARAKA RAJABU** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index **No. S3644/0068** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **FUNTA SECONDARY SCHOOL** mwaka **2013,** Cheti hiki kimepotea Mkoani **TANGA.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/39849/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SABRINA HAMAD ADAMU,** Anatangaza kupotelewa na Cheti cha Chuo chenye namba za Usajili IRDP/CCD/17/00425, Kilichotolewa na Chuo cha Mipango Dodoma Mwaka 2018 . Yeyote atakaekiona atoe taarifa klituo cha Polisi.
**TAARIFA YA POLISI: PHQ/DOD/DOD/60333/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SAID HAMDUNI JOSEPH**
anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 916 DPV aina ya NISSAN X-TRAIL. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu Taarifa ya polisi: **PHQ/SHI/KAH/12480/2024.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT COURT OF TANZANIA**
**AT KIOMBOI**
**CIVIL REVISION NO. 30090 OF 2024**
**WANDUTA MSENGI.........APPLICANT**
**VERSUS**
**REHEMA MOHAMEDI NGWIRA...............RESPONDENT**
**SUMMONS TO APPEAR**
**TO: REHEMA MOHAMEDI NGWIRA**
You are hereby commanded/ordered in the name of the United Republic of Tanzania to attend this court on the 6 day of January 2025 at 8:00 am in the above case and not to depart without leave of the court and you are hereby warned that if you shall without just excuse, neglect to obey this summons a warrant will be issued to compel your attendance, and you will furthermore render yourself liable to a fine as shall be determined by the Court.
GIVEN under my hand and the SEAL of the court this 16 day of December, 2024.

..................................
MAGISTRATE
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
IRAMBA DISTRICT COURT
KIOMBOI-IRAMBA

HABARIKIMATAIFA

# Mwanajeshi aongoza shambulizi la kigaidi ndani ya Marekani

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani Joe Biden amemuelezea mtu aliyehusika na shambulizi la risasi lililosababisha vifo vya watu 15 na wengine 15 kujeruhiwa kuwa amechochewa na kundi la kigaidi la Dola la Kiislamu (IS).

Shambulio hilo lilitokea katika mji wa New Orleans, nchini Marekani, mtu huyo aliyefahamika Shamsud-Din Jabbar, aliendesha gari na kuwagonga watu na kisha alichukua bunduki na kuwashambulia watu waliokusanyika barabarani kusheherekea mwaka mpya.

Akinukuu taarifa za Shirika la Upelelezi la Marekani FBI, Rais Biden alisema saa chache kabla ya shambulio hilo mhusika huyo alichapisha video kwenye mitandao ya kijamii, akielezea ana shauku ya kuua baada ya kuhamasishwa na IS.

Aidha, Rais Biden aliongeza kuwa vyombo vya usalama nchini humo, vinachunguza ikiwa kuna uhusiano wowote kati ya shambulio hilo na mlipuko uliotokea jana nje ya hoteli ambayo sehemu inamilikiwa na Rais mteule Donald Trump katika jiji la Las Vegas na kuua mtu mmoja.

Baada ya mlipuko huo, Trump alilihusisha tukio la mlipuko nje ya hoteli yake na wahamiaji haramu.

FBI imemtambua Shamsud-Din Jabbar, kuwa ni raia wa Marekani mwenye umri wa miaka 42 kutoka Texas. Wizara ya ulinzi ya Marekani Pentagon, ilisema Jabbar aliwahi kuhudumu katika jeshi kama mtaalamu wa rasilimali watu na mtaalamu wa Tehama kutoka mwaka 2007 hadi 2015 na kisha kikosi cha akiba hadi mwaka 2020.

Mtuhumiwa huyo mwenye cheo cha Staff Sajenti alikuwa miongoni mwa wanajeshi waliopelekwa Afghanistan kuanzia Februari 2009 hadi Januari 2010, kwa mujibu wa msemaji wa jeshi.

Mkuu wa Polisi wa New Orleans, Anne Kirkpatrick alimtaja Jabbar kama gaidi, huku FBI ikisema walikuta bendera ya IS ndani ya gari ambalo lilihusika kuvamia umati wa watu waliokuwa wanasherehekea Mwaka Mpya.

Maofisa wa usalama bado wanatafuta wahusika wengine wa shambuliz hilo, lakini hawakutoa maelezo ya kina huku ofisa mwanadmizi wa FBI, Alethea Duncan akionya kwamba hawaamini kuwa Jabbar alifanya uhalifu huo peke yake.

Shambulio hilo limetokea saa chache kabla ya jiji hilo kuandaa mchezo unaopendwa wa soka wa Sugar Bowl wa chuo kikuu.

Hata hivyo, mshambuliaji huyo aliuawa katika majibizano ya risasi na polisi baada ya kuwavamia watu.

Viongozi mbalimbali ulimwenguni wamelaani shambulizi hilo.


Kansela wa Ujerumani Olaf Scholz aliandika katika ukurasa wa X akisema ni taarifa ya kuhuzunisha kutoka New Orleans na kuongeza watu waliokuwa wakisherehekea kwa furaha wamevurugwa maisha yao au kujeruhiwa kwa chuki zisizo na maana.

Mshambulizi huyo aliendesha lori lenye rangi nyeupe na kufanikiwa kuingia mtaa wa Bourbon ambao ulijaa watu waliokuwa wakisherehekea Mwaka na kutekeleza mauaji hayo.

Watu walioshuhudia walisema kwamba lori hilo lilipitia vizuizi vilivyofunga barabara na kuwagonga watu.

Lori hilo la kubebea mizigo aina ya Ford 150 Lightning, limeelezwa kuwa lina injini yenye nguvu.

***DW***




Askari kutoka vyombo vya usalama vya Marekani wakiwa katika eneo kulikotokea shambulio la gari lililovamia umati wa watu mjini New Orleans jana. **PICHA: ALLIANCE**

# Waasi ADF waongeza mashambulizi DRC

**GOMA, DRC**

MASHAMBULIZI mapya ya wapiganaji wa kundi la waasi wa ADF linalodaiwa kuwa na mafungamano na kundi la kigaidi la Dola la Kiislamu, IS, yamesababisha vifo vya watu 12 mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Uvamizi huo ulifanyika baada ya mfululizo wa mashambulizi mengine ya ADF katika kipindi cha sikukuu ya Krismasi yaliyowaua watu 21 katika jimbo la Kivu Kaskazini. Maofisa wa eneo hilo walisema mashambulizi hayo yalitokea usiku wa kuamkia Jumatano na yalilenga maeneo mawili katika jimbo moja.

Ofisa mmoja, Samuel Kagheni, alilieleza shirika la habari la AFP kwamba waasi hao waliwaua watu wanane katika kijiji cha Bilendu.

Watu wengine wanne waliuawa katika kijiji cha Mangoya, huku waasi wakichoma moto nyumba katika maeneo yote mawili.

***DW***

## Rais wa Korea Kusini akataa kujisalimisha

**SEOUL, Korea Kusini**

RAIS aliyeondolewa madarakani wa Korea Kusini, Yoon Suk Yeol, amesisitiza hatajisalimisha kwa polisi kufuatia ombi la mahakama la kumtaka kukamatwa.

Kwa mujibu wa shirika la habari la Yonhap. Kiongozi huyo ambaye bado anashikilia rasmi wadhifa wake, alieleza hawezi kukubali kukamatwa na ataendelea kupambana hadi mwisho.

Yoon Suk ndiye rais wa kwanza aliye madarakani katika historia ya Korea Kusini kuwahi kupewa hati ya kukamatwa baada ya kuhusika na kutoa amri ya sheria ya kijeshi inayohesabika kama kitendo cha uasi na matumizi mabaya ya kijeshi.

Rais Yoon alitakiwa kuhojiwa, lakini hakutokea alipoitwa na timu inayochunguza sakata hilo.

Ofisi Kuu ya Upelelezi wa Ufisadi (CIO), ambayo inafanya uchunguzi wa suala hilo, inatakiwa kutekeleza amri hiyo ya mahakama hadi Januari 6 .

***RFI***

## Iran yaionya Marekani kuhusu Syria

**TEHRAN, Iran**

KIONGOZI Mkuu wa Iran, Ayatollah Ali Khamenei, amekosoa uwepo wa vituo vya kijeshi nchini Syria.

Akizungumza katika kumbukumbu ya kuuawa kwa Jenerali Qassem Soleimani, Khamenei alisema

Syria itabaki kuwa ya Wasyria wenyewe, na yeyote atakayeshambulia ardhi yake bila shaka atalazimika kuondoka mbele ya upinzani wa vijana wa nchi hiyo.

Aliongeza kuwa,kambi za Marekani nchini Syria bila shaka zitaharibiwa na vijana wa Syria.

Kiongozi huyo alisema iwapo nchi yake itaondoa vipengele vya uthabiti na nguvu zake kwenye medani, itakuwa rahisi kukaliwa kama inavyotokea kwa Syria.

Alisema Marekani, Israel na baadhi ya nchi za kikanda zimeigawanya Syria ambayo kwa sasa haina nguvu tena.

# Gets Program Queens yatema wachezaji tisa

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Gets Program ya jijini, Dodoma inayoshiriki Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (TWPL), imetangaza rasmi kuachana na wachezaji tisa katika kipindi cha dirisha dogo lililofunguliwa, imethibitishwa.

Wachezaji hao wameachwa kwa sababu mbalimbali, mojawapo ikiwa ni klabu kushindwa kutimiza matakwa ya mkataba waliyokubaliana na nyota hao wakati wanasajiliwa.

Lakini kutokana na changamoto ya kiutawala inayoikabili timu hiyo, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), limelazimika kusimamisha michezo yake ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, ambayo inaendelea hapa nchini.

Taarifa rasmi iliyotolewa na klabu hiyo yenye makazi yake jijini, Dodoma imewataja wachezaji waliochana nao ni Zubeda Mgunda, Zainabu Mohammed 'Dudu', Koku Kipanga, Diana Mnally, Janeth Nyagali, Anandez Lazaro, Nasmah Manduta, Lucy Mrema na Elizabeth Nashon.

"Tunapenda kutoa taarifa kwa umma tumeachana na wachezaji tisa, bado hatujatangaza wapya watakaochukua nafasi ya wachezaji walioondoka katika kikosi chetu," ilisema sehemu ya taaifa ya klabu hiyo.

Iliongeza inawatakia kila la heri katika changamoto mpya huko wanakokwenda.

Tayari Zubeda na Dianna wameshajiunga na Yanga Princess huku Zainab akisajiliwa na Mashujaa Queens, zote za Dar es Salaam.

Mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania umemalizika na hatua ya lala salama inatarajiwa kuanza ifikapo Januari 21, mwaka huu.

Mabingwa watetezi, Simba Queens yenye pointi 25 ndio inaongoza ligi hiyo ikifuatiwa na JKT Queens yenye pointi 20 lakini ikicheza mechi moja pungufu ukilinganisha na vinara hao huku Mashujaa Queens ikifuatia baada ya kujikusanyia pointi 15 na Yanga Princess yenye pointi 12 ikishika nafasi ya nne.

Tano Bora katika ligi hiyo inayoshirikisha timu 10 inakamilishwa na Alliance Girls ya jijini Mwanza yenye pointi 11 na Mlandizi Queens kutoka mkoani, Pwani yenye pointi moja ikiburuza mkia.

Bingwa wa ligi hiyo hupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), yenye lengo la kusaka tiketi ya kufuzu michuano ya Fainali ya Ligi ya Mabingwa kwa Wanawake Afrika.

# CAMARA BADO 'CLEAN SHEET' 3 ILI KUMFIKIA LEY MATAMPI

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA namba moja wa Simba, Moussa Camara, raia wa Guinea, amebakisha 'clean sheets' tatu ili kuzifikia za aliyekuwa mlinda mlango Mkongomani, Ley Matampi, ambaye alipata katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita akiwa na Coastal Union.

Taarifa iliyotolewa jana na Bodi ya Ligi inasema Camara amesimama langoni mara 12 bila kuruhusu wavu wake kuguswa, hivyo kuongoza kwa 'clean sheets' kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara iliyomaliza mzunguko wa kwanza, ikiwa imesimama kupisha michuano ya Kombe la Mapinduzi na Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa wachezaji wa ndani (CHAN), inayotarajiwa kufanyika mwezi ujao hapa nchini, Kenya na Uganda.

Rekodi za dawati la michezo, Nipashe, zinaonyesha kipa aliyemaliza kinara wa kukaa langoni mara nyingi zaidi bila kuruhusu Ligi Kuu msimu uliopita alikuwa ni Matampi aliyekuwa imara zaidi katika michezo 15 ya ligi hiyo.

Kwa maana hiyo, Camara aliyesimama langoni katika michezo yote 15 ambayo Simba imecheza mzunguko wa kwanza, amebakisha tatu tu kumfikia, huku akiwa na mechi nyingine 15, akiwa na asilimia nyingi za kuendelea kukaa langoni.

Matampi, aliichezea Coastal Union msimu huu kwa nusu msimu na wakati dirisha la usajili linafunguliwa, alivunja mkataba kwa makubaliano na klabu yake, huku taarifa zinasema huenda akatimkia Tabora United.

Wakati Camara, akiendelea kuwatesa makipa wa Ligi Kuu kwa 'clean sheets', anayefuatia ni Patrick Munthali wa Mashujaa FC ya Kigoma ambaye ana nane Clean Sheet mpaka sasa.

Makipa wanaoshika nafasi ya tatu kwa kukaa michezo mingi bila wavu wao kuguswa ni, Djigui Diarra wa Yanga, raia wa Mali, na Metacha Mnata wa Singida Black Stars ambao wana 'clean sheets' saba kila mmoja, huku Mohamed Mustafa wa Azam FC, raia wa Sudan, akiwa nazo sita.

Makipa wengine ni Yacoub Suleiman wa JKT Tanzania na Yona Amosi wa Pamba Jiji, wamekaa langoni bila kuruhusu wavu kuguswa mara tano mpaka sasa.

Wakati huo huo, straika wa Singida Black Stars, Elvis Rupia, bado yupo kileleni mwa orodha ya wapachika mabao kwenye Ligi Kuu akiwa na mabao manane mpaka sasa, akifuatiwa na kiungo mshambuliaji wa Simba, Jean Ahoua, mwenye mabao saba.

Kwa mujibu wa takwimu, Selemani Mwalimu wa Fountain Gate na Clement Mzize wa Yanga wote wa mabao sita, huku Leonel Ateba wa Simba, Edgar Willliam wa Fountain Gate, Pacome Zouzoua na Prince Dube wa Yanga na Peter Lwasa wa Kagera Sugar, wote wana mabao matano kila mmoja.



Wachezaji wa Timu ya Kituo cha Shirikisho la Soka Tanzania (TDS) wenye umri chini ya miaka 17 wakifanya mazoezi ili kujiandaa na mashindano ya Afrika kwa Wasichana (GIFT), yatakayofanyika kuanzia Januari 7 hadi 18, mwaka huu jijini, Dar es Salaam kwa kushirikisha timu kutoka Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA). **PICHA: TFF**

# Azam yaandaa kliniki ya vijana

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Azam unatarajia kuendesha mafunzo maalumu ya wachezaji chipukizi wenye umri kati ya miaka saba na 15, yatakayofanyika kesho na keshokutwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa Vijana wa timu hiyo, Kassim Liogope, alisema wanawakaribisha watoto kutoka sehemu mbalimbali kushiriki mafunzo hayo ambayo yatakuwa msingi katika kukuza vipaji vyao.

Liogope alisema mafunzo yao yatakuwa maamulu kwa ajili ya kuwaandaa watoto kiufundi.

Alisema mafunzo hayo yatakuwa na sehemu mbili, darasani na baadaye watahamia uwanjani.

"Hii ni kliniki maalumu kwa ajili ya vijana wadogo, itaongozwa na makocha wa Azam, na mafunzo yetu yatajikita sana masuala ya ufundi, ni namna gani mtoto anafundishwa misingi ya mpira wa miguu," Liogope alisema.

Aliongeza watoto wote watakaoshiriki mafunzo hayo watapatiwa vyeti maalumu, jezi pamoja na bidhaa mbalimbali zinazozalishwa na Kampuni ya Bakhresa.

Azam FC, mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa mwaka 2014/2015, ikiongozwa na nahodha, John Bocco na Kocha Mkuu, Stewart Hall, imekuwa na utaratibu wa kufanya mafunzo hao kila mwaka na baadhi ya watoto wenye vipaji hubakia katika klabu hiyo kuendelea na mfunzo na baadaye kuzitumikia timu zao vijana.

## ZISIKUPITE

### UNITED YAMTAKA GYOKERES

KLABU ya Manchester United itajaribu kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Sweden, Viktor Gyokeres, mwenye umri wa miaka 26, kutoka Sporting mwezi huu. ***(Mirror)***

### TRENT AKARIBIA MADRID

REAL Madrid inaendelea na mkakati wa kumsajili, Trent Alexander-Arnold, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 akitafuta njia za kuondoka Liverpool. Klabu hiyo ya LaLiga inamtaka beki huyo wa England kusaini mkataba wa awali. ***(Relevo)***

### MARMOUSG AGEULA LULU

KLABU ya Arsenal inaongoza katika kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Eintracht Frankfurt, ambaye ni raia wa Misri, Omar Marmoush, mwenye umri wa miaka 25, huku Liverpool, Paris St-Germain na AC Milan zikiwa zimeonyesha nia ya kumhitaji nyota huyo. ***(GiveMeSport)***

### DECO AMCHAGUA DIAZ

NIA ya mkurugenzi wa michezo wa Barcelona, Deco kumsajili winga wa Liverpool kutoka Colombia, Luis Diaz imeongezeka, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 akiwa hana furaha kufuatia kutoanza kwa mazungumzo kuhusu kuboreshwa kwa mkataba wake pale Anfield. ***(Sport)***

### TRAFFORD KUTUA NEWCASTLE

NEWCASTLE United inapanga kumnunua kipa wa Burnley mwenye umri wa miaka 22, James Trafford, kwa kitita cha pauni milioni 20. ***(Sun)***

### DONSO ANUKIA WOLVES

KLABU ya Wolves inataka kumsajili mlinzi wa Lens na Timu ya Taifa ya Austria, Kevin Danso, mwenye umri wa miaka 26 katika dirisha dogo la usajili Januari hii. ***(Sky Sports)***

### MC-ATEE SOKONI ULAYA

BAYERN Leverkusen ni miongoni mwa klabu kadhaa zinazomtazama kwa karibu kiungo wa kati wa Manchester City, mwenye umri wa miaka 22, James McAtee. ***(Mail)***

### WERNER KUREJEA LEIPZIG

KLABU ya Tottenham Hotspur haina uwezekano wa kubadilisha mkataba wa mkopo wa mshambuliaji wa Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 28 na kuwa mkataba wa kudumu, na hiyo inamaana atarejea RB Leipzig msimu wa kiangazi ***(Bild)***

### SAINZ KWENDA ATHLETIC

ATHLETIC Bilbao imemtambua kiungo wa kati wa Norwich, Borja Sainz, mwenye umri wa miaka 23, kama kiungo mbadala bora wa Nico Williams (22), iwapo winga huyo wa Hispania ataondoka katika klabu hiyo msimu wa kiangazi. ***(Sport)***

### WOOD KUHAMIA SERIE A

AC Milan na Napoli ni miongoni mwa klabu ambazo zinaweza kumnunua mshambuliaji wa Nottingham Forest, Chris Wood mwenye umri wa miaka 33 , iwapo mchezaji huyo wa kimataifa wa New Zealand atashindwa kukubaliana na klabu hiyo kuhusu mkataba mpya. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MOURINHO : NINAJUTIA KUREJEA CHELSEA 2013

●●● Kocha huyo Mreno asema uamuzi huo ulivunja mahusiano yake...

**ROME, Italia**

JOSE Mourinho amekiri uamuzi wa kuondoka Real Madrid mwaka 2013, ili kujiunga tena na Chelsea, ni miongoni 'mambo makubwa' anayojutia katika maisha yake ya soka.

Mreno huyo alifika njia panda mwaka 2013, msimu mmoja pekee ndani ya mkataba wake wa miaka minne huko Real Madrid, lakini akitoka kwenye kampeni iliyojiita "mbaya zaidi" katika maisha yake ya soka.

Mourinho, ambaye hatimaye alivunja utawala wa Barcelona wa La-Liga kwa msimu mzuri wa pointi 100 wa mwaka 2011/2012, aliondoka Madrid na kurudi katika mikono ya Chelsea kwa kipindi cha pili huko London.

Hiyo ilimaanisha kumwambia Rais wa Madrid, Florentino Perez, anataka kutoka na kuvunja mahusiano.

Katika mahojiano na chapisho la Roma la Corriere dello Sport wiki hii, kocha huyo mwenye umri wa miaka 61 alisema anajutia sana hilo.

"Tukizungumzia mechi, sana kwa sababu unapopoteza huwa unafikiri ungeweza kufanya tofauti, na mimi nimepoteza mechi nyingi," alijibu.

"Ikiwa unarejelea chaguzi za kitaaluma, 'hapana' kwa Florentino. Aliniambia, 'Mou, usiondoke sasa, umefanya sehemu ngumu na sehemu nzuri bado inakuja.' Nilijua. ingekuwa hivi, lakini nilitaka kurejea Chelsea baada kukaa Hispania miaka mitatu ya mapambano makubwa."

Ingawa Mourinho aliipa Chelsea taji la Ligi Kuu msimu wa 2014/15, la kwanza kwa klabu hiyo katika kipindi cha miaka mitano, Madrid mara moja walishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya bila yeye.

Pia alisema majuto yake mengine makubwa yalikuwa kutoondoka Roma mapema, mara baada ya huzuni ya kupoteza fainali ya Ligi ya Europa 2023 kwa mikwaju ya penalti dhidi ya Sevilla.

## Olmo anataka kubaki Barcelona

**BARCELONA, Hispania**

WAKALA wa Dani Olmo amesisitiza kiungo huyo hana nia ya kuondoka Barcelona Januari hii licha ya sintofahamu inayoendelea kuhusu usajili wake.

Usajili wa sasa wa Olmo kwenye LaLiga ulimalizika mwishoni mwa Desemba na klabu hiyo kwa sasa haiko katika nafasi ya kumsajili tena mchezaji huyo, ambaye mkataba wake unaaminika kuwa na uwezo wa kuondoka kwa uhamisho wa bure ikiwa hawezi kusajiliwa na timu kadhaa za Ligi Kuu England zinamwania.

Barcelona wametokwa na jasho baada ya kuona jaribio la kuongeza muda wa usajili wa Olmo limekataliwa na majaji wawili tofauti, maana yake ni saa chache kabla ya nyota huyo wa kimataifa wa Hispania kutokuwa sehemu ya kikosi tena.

Hata hivyo, wakala wa Olmo, amesisitiza bado mteja wake anataka kubaki.

"Naweza kutangaza uamuzi uliofanywa na Dani ni kubakia Barcelona," alisema akimwambia Fabrizio Romano.

"Hatuzingatii chaguo lingine au klabu, Dani Olmo anataka kuichezea Barca na nia yake iko wazi."

Habari za kutaka Olmo kusalia bila shaka zitapunguza wasiwasi kuhusu Barcelona, ambao wanaamini kuwa wana njia tofauti ya kukusanya fedha zinazohitajika tayari.

## Vinicius, Mbappe wajitabiria makubwa 2025

**MADRID, Hispania**

NYOTA wa Real Madrid, Vinicius Junior na Kylian Mbappe wana matumaini kuhusu mwaka 2025, sasa wamebakiwa na nusu msimu kuzoeana.

Mbappe hakufika Madrid akiwa na utimamu wa hali ya juu baada ya kupumzika kidogo kufuatia Euro 2024 na hivi karibuni ameanza kupiga hatua.

Mfaransa huyo alikiri ilikuwa tabu kukosa penalti mapema Desemba dhidi ya Athletic Club, hali hiyo ilimvuruga sana.

Vini kwa ujumla alikuwa katika kiwango kizuri lakini alikosa mechi kadhaa Desemba kutokana na jeraha.

Madrid wapo nyuma kwa pointi moja tu dhidi ya vinara wa LaLiga, Atletico.

"Kylian ni mchezaji mkubwa na mtu mzuri. Ni rahisi sana kucheza naye. Atafunga mabao mengi kwa Madrid. Huu ni mwanzo tu," alisema Vini.

Mbappe alitoa kauli kama hizo, akizungumza vyema kuhusu kile kitakachokuja.

"Tunaweza kufunga mabao mengi zaidi na tutafanya hivyo. Ilinibidi kuzoea timu mpya na chumba cha kubadilishia nguo kimenisaidia sana. Ninawashukuru wote," alisema mchezaji huyo wa zamani wa Paris Saint-Germain.

"Ni nini ninachopenda zaidi kuhusu Vini? Unyenyekevu wake, bila shaka.

"Kila mtu anamfahamu mchezaji huyo na anaona ubora alionao kila baada ya siku tatu, mwaka huu ameshinda mataji mengi ya pamoja na tuzo binafsi, lakini naangazia unyenyekevu wake. Yeye huwa anaelewana vizuri na watu kwenye chumba cha kubadilishia nguo na napenda hivyo.



# AMORIM: UNITED HATUSAJILI JANUARI

**MANCHESTER, England**

RUBEN Amorim amesema hatarajii kuongezewa nguvu katika kikosi chake katika dirisha dogo la usajili la Januari anapojaribu kuzuia hali ya wasiwasi ya Manchester United kuelekea nafasi za kushuka daraja.

Kichapo dhidi ya Newcastle kwenye Uwanja wa Old Trafford mapema wiki hii kilikuwa cha nne mfululizo kwa United katika mashindano yote na imeiacha timu ya Amorim katika nafasi ya 14, pointi saba pekee kutoka kwa eneo la kushuka.

Moja ya masuala yanayomkabili kocha huyo wa Ureno ni ukosefu wa wachezaji wanaoendana na mfumo wake wa 3-4-3, lakini hatarajii klabu kutumia fedha kurekebisha hilo wakati wa dirisha dogo la la usajili.

"Hatuna uwezekano huo," alisema Amorim.

"Unajua hali vizuri kuliko mimi. Siyo sifiki hapa na ninaweza kutumia fedha nyingi, kubadilisha timu yote. Unajua hali hiyo kwa hiyo sio maana kuizungumzia."

Vyanzo vimeiambia ESPN ambayo biashara yoyote United itafanya mnamo Januari itategemea wachezaji kuondoka. Klabu iko wazi kwa uhamisho wa kudumu au kwa mkopo na ikiwa fedha itapatikana beki mpya wa kushoto atakuwa kipaumbele.

Amorim tayari anakabiliwa na maswali kuhusu kama anafaa kubadili mfumo wake kwa wachezaji alionao.

Lakini kocha huyo mwenye umri wa miaka 39 amesisitiza atabakia na mfumo wa 3-4-3 anapojiandaa kwa safari ngumu kuelekea Anfield kumenyana na vinara wa Ligi Kuu England, Liverpool hapo Jumapili.

"Lazima niuze wazo langu," alisema.

"Nikibadilika kila wakati itakuwa mbaya zaidi. Lakini ninaelewa wana shida sana kwa sababu walitumia miaka miwili kucheza njia moja. Unaweza kuhisi, naweza kuhisi lakini lazima niuze wazo langu."

## HABARI MICHEZO

# ZANZIBAR HEROES, KILI STARS KIBARUANI MAPINDUZI CUP

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WENYEJI Timu ya Soka ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes), inatarajia kuikaribisha Tanzania Bara (Kilimanjaro Stars), katika mechi ya ufunguzi ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi (Mapinduzi Cup 2025), itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Gombani, Pemba.

Mashindano hayo mwaka huu yanashirikisha timu za taifa badala ya klabu kama ilivyozoeleka, na mataifa yaliyothibitisha kuleta vikosi vyao wanatumia michuano hiyo kujiandaa na Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Kocha Msaidizi wa Zanzibar Heroes, Ali Suleiman Mtuli, alisema jana wamejiandaa vyema kuelekea mashindano hayo na wanaamini huu ni wakati wao wa kuwapa furaha Wazanzibar.

Mtuli alisema wachezaji wake wako tayari na mechi hiyo ya ufunguzi na itakuwa ngumu kutokana na historia ya timu hizo zinazokutana.

„Tunajua itakuwa mechi ngumu lakini tumejipanga kuhakikisha tunapata ushindi siku ya kesho (leo), Mechi yetu na Tanzania Bara haijawahi kuwa rahisi kuanzia mashabiki mpaka wachezaji," alisema Mtuli.

Naye nahodha msaidizi wa timu hiyo, Ahmed Ali Suleiman ‚Salula', alisema wachezaji wako tayari kwa ajili ya kupeperusha vyema bendera ya Zanzibar katika michuano hiyo.

Alisema kikosi chao kimepata muda mzuri wa kujiandaa na mashindano hayo na wanaamini hawatawaangusha mashabiki wao.

„Wachezaji tupo vizuri , hamasa ni kubwa kwetu na muda tuliopata wa kufanya mazoezi ya pamoja imekuwa ni sababu ya sisi kuwa na hamu ya kupata matokeo bora. Tuna deni kubwa kwa mashabiki wa Zanzibar Heroes, lakini niwaombe waje kwa wingi uwanjani kutupa hamasa zaidi ya kupata ushindi," Salula alisema.

Mashindano hayo yataendelea kesho kwa Kenya (Harambee Stars), kuikabili Burkina Faso na Januari 6, mwaka huu Burkina Faso itacheza dhidi ya Zanzibar Heroes na siku inayofuata Kilimanjaro Stars iliyoko chini ya Kocha Mkuu, Hamad Ally, itawaalika Kenya.

Fainali za mashindano hayo zitafanyika Januari 13, mwaka huu.



Wachezaji na baadhi ya viongozi wa benchi la ufundi wa Yanga Princess ya Dar es Salaam wakishangilia baada ya mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (TWPL), dhidi ya Ceasiaa Queens iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Samora mkoani, Iringa juzi kumalizika. Yanga Princess ilipata ushindi wa mabao 4-1. **PICHA: MTANDAO**

# Tabora United: Asanteni wageni

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Tabora United inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara imesema mafanikio waliyopata msimu huu yanatokana na ‚mchango mkubwa' wa wachezaji wa kigeni waliowasajili tofauti na timu nyingine nyota wao wa kulipwa wanakosa namba katika kikosi cha kwanza, imeelezwa.

Tabora United imesajili wachezaji wageni 12, na wakati mwingine nyota hao wote wanapata nafasi ya kucheza na kuisaidia timu kufikia malengo.

Akizungumza baada ya kukamilika kwa mzunguko wa kwanza, Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Christina Mwagala, amesifia usajili wao ‚umelipa' na pia amewapongeza wachezaji hao wa kigeni kuzoea haraka mazingira ya soka la Tanzania.

"Nadhani sisi Tabora United ndiyo tuna wachezaji 12 ya kigeni ambao wanacheza wote, yaani kuna mechi wanaweza kucheza wote 12, waanza baadhi halafu kipindi cha pili wanaingia wengine, Hii ni kwa sababu hatukukurupuka katika usajili, timu nyingine mechi inaisha wachezaji watano au saba tu wageni ndio wamecheza, kwa sababu wengine viwango vyao ni vya kawaida sana na wanazidiwa na wachezaji wa hapa Bongo," Mwagala alisema.

Hata hivyo Mwagala alisema haina maana wachezaji wao wazawa hawana ubora, ila wote wanachuana kwa ajili ya kushawishi mwalimu kuwapa nafasi.

"Ndiyo maana utaona wachezaji wa kigeni wa Tabora United wote wanacheza na Watanzania kama, Offen Chikola pia wanacheza kwa kiwango cha juu, kwa sababu huwa tunasajili kwa kuangalia viwango na si utaifa," aliongeza ofisa huyo.

## Yanga: Ama zao, ama zetu

INATOKA UK. 24

ganda wala siasa, hatukuanza vizuri michuano hii, sasa tunahitaji pointi tatu ili tuinuke, tutoke mwisho wa msimamo, sisi ni timu kubwa haiwezekani tuendelee kukaa huko," Kamwe alisema.

Kuhusu maandalizi alisema, Kocha Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, ameendelea kukinoa kikosi na kuangalia wachezaji ambao anaweza kuwatumia katika mechi hiyo huku waliokuwa majeruhi wakianza kujifua pamoja na wenzao.

„Golikipa wetu Djigui Diarra, Maxi Nzengeli na Clatous Chama wameshaanza mazoezi na kikosi kwa ajili ya mchezo huo, ila Yao Kouassi bado afya yake na utimamu wa mwili haujakuwa sawa, hajaanza mazoezi, hivyo hatakuwa sehemu ya kikosi," alisema Kamwe.

Kikosi cha TP Mazembe kilitarajiwa kutua nchini jana jioni, tayari kwa ajili ya mchezo huo wa raundi ya nne, baada ya kutoka sare ya bao 1-1 mjini Lubumbashi, hapo Desemba 14, mwaka jana.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara walianza hatua hiyo ya makundi kwa kupokea kichapo cha mabao 2-0 hapa nyumbani kutoka kwa Al Hilal na ikiwa ugenini kufungwa idadi kama hiyo na MC Alger ya Algeria.

## Simba: Tuko salama Tunisia, tunajipanga

INATOKA UK. 24

Mohamed Hussein ‚Zimbwe Jr' amesema wachezaji wote wako katika hali nzuri na wanatarajia kupambana kuhakikisha wanapata matokeo chanya.

"Tumekuja kwa ajili ya mchezo wa Kombe la Shirikisho ndani ya uwanja kwa dakika 90, hatuna hofu, mpaka sasa hakuna chochote, najua hakuna chochote kibaya kitakachotokea, pia sisi hatuogopi chochote, ni wazoefu sana katika michuano ya kimataifa na tumeshakutana na mambo mengi ndani na nje ya uwanja.

Sisi tumekuja kucheza mpira, hayo mambo mengine huwa yanatokea tu bila kupangwa, ukiangalia hata siku ile mashabiki wao walianzisha vurugu kwa sababu hawakupata matokeo waliyotarajia ya sare ambayo tayari wao walishajua wameipata," alisema beki huyo wa kushoto.

Hata hivyo, SC Sfaxien imepigwa marufuku kuingiza mashabiki kutokana na kufanya fujo katika mchezo wao dhidi ya CS Constantine ambao walipoteza kwa kufungwa bao 1-0, mechi iliyochezwa Novemba 27, mwaka jana.

Huenda klabu hiyo ikakumbana na rungu lingine kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), kufuatia baadhi ya viongozi wa benchi la ufundi, wachezaji na mashabiki kufanya vurugu katika mchezo dhidi ya Simba uliochezwa Desemba 15, mwaka jana.

Baada ya mechi hiyo, Simba itajipanga kuwafuata Bravos do Maquis na itamaliza mechi za hatua ya makundi nyumbani kwa kuwakaribisha CS Constantine kutoka Algeria.

Michezo
Ijumaa Januari 3, 2025
Nipashe

## Mourinho : Ninajutia kurejea Chelsea

UKURASA 21





# Yanga: Ama zao, ama zetu

Vigogo hao wasema TP Mazembe ndio daraja lao la kutinga...

**Na Adam Fungamwango**

WAWAKILISHI pekee wa nchi katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Yanga wamesema mechi dhidi ya TP Mazembe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo), itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam ni daraja lao la kuvuka kwenda hatua ya robo fainali ya michuano hiyo ya kimataifa.

Yanga pia imesema haivutii kuona timu yao inashika nafasi ya mwisho katika msimamo wa Kundi A ikiwa na pointi moja tu huku kinara akiwa ni Al Hilal ya Sudan yenye pointi tisa.

Akizungumza jijini jana, Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema wamekaa na wachezaji na kukubaliana mechi ya kesho watacheza kama hakuna mchezo mwingine watakaocheza tena kwa sababu ndio utakuwa daraja la wao kwenda hatua mbele ya michuano hiyo, vinginevyo watakuwa wamejiweka katika hali mbaya.

Kamwe alisema wakati wachezaji wakihamasishana ‚kufia uwanjani' katika mechi hiyo, amewataka mashabiki wa Yanga kujitokeza kwa wingi kwa ajili ya kuwashangilia na kuwapa hamasa na kuufanya Uwanja wa Benjamin Mkapa uwe kama ‚tanuri la moto' kwa wapinzani.

Alisema haipendezi kwa klabu kama Yanga ambayo msimu uliopita ilifika hatua ya robo fainali ishike mkia katika kundi kutokana na kuvuna pointi moja pekee baada ya kucheza michezo mitatu.

"Wanachama na mashabiki wa Yanga, naweza kutumia maneno mengi ili kujua mchezo huu una umuhimu mkubwa kwetu. Ukweli ambao utaendelea kubakia na hatuwezi kuuepuka na unatuonesha kwa picha inayoumiza ni pale tunapolitazama kundi letu, haipendezi na haivutii, lakini ndiyo ukweli, kwenye kundi letu tuna pointi moja tu, ambayo tumeipata katika michezo mitatu. Ukweli huo hauishii hapo, bali tunashika nafasi ya mwisho," alisema Kamwe.

Aliongeza ukweli huo ndiyo iwe chachu kwa Wanayanga kufanya kitu kwa ajili ya timu yao, na hakuna kingine ila kujitokeza kwa ajili ya kuujaza uwanja kwa lengo la kuwatoa mchezoni TP Mazembe.

"Ukweli huu mchungu unapaswa kuwa hamasa namba moja kwa kila Mwanayanga anapoufikiria mchezo huo. Nasema ukweli mchungu kwa sababu hauhitaji propa-

INAENDELEA UK. 23

## Simba: Tuko salama Tunisia, tunajipanga

**Na Adam Fungamwango**

TOFAUTI na ilivyotarajiwa, uongozi wa Simba umesema msafara wao haujapata changamoto wala kufanyiwa figisu ya aina yoyote baada ya kuwasili nchini Tunisia kuwafuata wenyeji, CS Sfaxien kwa ajili ya mechi ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, imethibitishwa.

CS Sfaxien itawakaribisha Simba katika mechi ya raundi ya nne ya Kundi A itakayochezwa keshokutwa kuanzia saa 1:00 usiku kwa saa za Tanzania kwenye Uwanja wa Olympique Hammadi Agrebi.

Katika mchezo uliozikutanisha timu hizo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, mashabiki wa CS Sfaxien walianzisha vurugu kufuatia Simba kupata bao la dakika za ‚jioni' lililofungwa na Kibu Denis, wenyeji wakapata ushindi wa mabao 2-1, ambapo viti kadhaa vya uwanja huo viling'olewa.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema mashabiki na wanachama wa klabu hiyo wasiwe na wasiwasi wowote kwa sababu wal-



itua Tunisia salama na hawakukutana na changamoto yoyote kuanzia kwenye uwanja wa ndege hadi hotelini, sehemu ambazo mara nyingi dalili za figisu za soka huanzia hapo.

Ahmed alisema wamejitahidi kukwepa kila eneo ambalo wanadhani wangeweza kufanyiwa hujuma kwa kushirikiana na ubalozi wa Tanzania nchini Tunisia.

"Tumewasili salama baada ya safari ndefu, tumefika hapa hakuna changamoto yoyote, shauku imekuwa ni kubwa na hofu imekuwa kubwa hasa kwa Wanasimba wakioanisha na kile ambacho kilitokea katika mechi ya kwanza, pengine wakidhani ingeweza kutusumbua baada ya kufika hapa, niwaambie kila kitu kimekwenda vizuri.

Muda tuliokaa uwanja wa ndege ni ule ambao unatumiwa na viwanja vyote, maana yake hakukuwa na vigisu yoyote ile, lakini haya yote tumeyafanya kwa kushirikiana na Ubalozi wa Tanzania nchini Tunisia, kila kitu kimekwenda vizuri," alisema Ahmed.

Kuhusu hali ya hewa, Ahmed alisema ni baridi lakini siyo kama ile waliyokutana nayo nchini Algeria walipokwenda kucheza dhidi ya CS Constantine.

Naye nahodha msaidizi wa timu hiyo,

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >